TGNP

TGNP

HerStory

Wanawake Walioshika Usukani

Simulizi zenye hamasa kuhusu viongozi mahiri wanawake

Wanawake Walioshika Usukani

© Mtandao wa Jinsia Tanzania(TGNP), 2020

Yaliyomo

Kuhusu TGNP i
Dibaji iii
Utangulizi 1
Muktadha 3
Hadithi/Simulizi 6

Kuhusu TGNP

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni asasi ya kiraia ambayo ilianzishwa mwaka 1993. Chimbuko la TGNP ni mchakato wa majadiliano na tafakuri ya pamoja kati ya wanaharakati, wanazuoni pamoja na viongozi wa mashirika ya wanawake yanayohamasisha usawa wa jinsia, haki za wanawake pamoja na ukombozi wa wanawake. Tafakuri na majadiliano hayo yaliaanza miaka ya tisini wakati ambapo sera za utandawazi na urekebishaji wa uchumi zimeshika kasi duniani kote. Sera hizi zilisababisha ubinafsishaji na uchangiaji wa huduma za jamii ambapo wanawake na wanaume masikini walipata changamoto katika kumudu huduma hizo. Hali hii iliongeza kazi ya kujenga madaraja na kuongeza pengo la walionacho na wasionacho huku waathirika wakubwa wakiwa ni wanawake, vijana na wanaume masikini.

Kipindi hicho pia kulikuwa na maandalizi ya mkutano wa nne wa dunia wa wanawake uliofanyika huko Beijing -China mwaka 1995. Mkutano huu ulitanguliwa na mikutano mitatu ambayo ni Mkutano wa kwanza wa wanawake wa dunia uliofanyika Mexico mwaka 1975, Mkutano wa pili ulifanyika Copenhagen-Denmark mwaka 1980, na Mkutano wa tatu ulifanyika Nairobi Kenya mwaka 1985. Mikutano yote hii ilikuwa na madhumuni ya kuweka mikakati ya jinsi ya kuendeleza usawa wa jinsia na haki za wanawake duniani.

Maandalizi ya Mkutano wa Beijing hapa nchini ulihusisha majadiliano kuhusu hali halisi ya wanawake Tanzania kisiasa, kiuchumi na kijamii yakiangalia mafanikio, changamoto na nini kifanyike kutatua changamoto hizo. Michakato huo uliimarisha nguvu za pamoja katika kutafakari, kushirikishana uzoefu, kukubaliana masuala muhimu na mikakati ya jinsi ya kusonga mbele katika kuendeleza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake. Vile vile mchakato huo ulizalisha chapisho la kwanza la "Hali Halisi ya Jinsia Tanzania 1995" pamoja na taarifa za pamoja ambazo ziliwekwa pamoja na Taarifa nyingine za Afika ambazo ziliwasilishwa kama sauti ya pamoja ya wanawake wa Afrika. Kutokana na mafanikio makubwa ya mchakato huu ilionekana kwamba inapaswa kuwa na chombo au taasisi ya kuratibu harakati hizo za ujenzi wa nguvu za pamoja ili kuleta usawa wa kijinsia, haki za wanawake na zile za kijamii hapa nchini na nje ya nchi. Hapo ndipo Mtandao wa Jinsia Tanzania ulizaliwa rasmi 1993.

Dira ya TGNP ni kuwa na jamii ya kitanzania yenye kuzingatia usawa wa kijinsia, haki, uwezeshaji wa wanawake na haki za kijamii.

Utume wa TGNP ni kujenga vuguvugu la harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi lenye lengo la kuleta mabadiliko ya kijinsia na uwezeshaji wanawake nchini.

Lengo kuu la TGNP ni kuwa chachu ya ujenzi wa vuguvugu la harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi kwa njia ya uraghbishi na uchechemuzi ili kuwezesha jamii husika kudai mabadiliko katika mifumo, sera na utengaji sawa na wa haki wa rasilimali katika ngazi zote kwa mtizamo wa kijinsia

Dibaji

Tunayo furaha kubwa kuwasilisha kwenu kitabu hiki kinachojulikana kama "*Wanawake Walioshika Usukani: Simulizi za Viongozi Mahiri Wanawake*". Kitabu hiki kimeandaliwa na TGNP kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo kutoka nchini Norway lijulikano kama Norad kwa lengo la kuchangia katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa kupitia uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 .

Kuandika simulizi/kestoria zenye kuonesha michango ya wanawake katika maendeleo kupitia nafasi zao mbalimbali za uongozi ni moja ya mikakati ya TGNP ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali za uongozi. Mkakati huu umeonesha mafanikio makubwa hususani katika kuwavutia vijana wanaochipukia pindi wanaposoma kestoria hizo ambazo zimesheheni mbinu mbalimbali walizotumia wanawake hao mahiri kuwawezesha kuibuka kidedea katika nafasi zao za uongozi. Vijana wengi walipata mwamko na kuamua kutia nia kwa kusoma tu hizo simulizi. Ni ukweli usiofichika kuwa wanawake wamekuwa mahiri na kuchangia maendeleo kwa njia mbalimbali lakini michango yao haijaandikwa na wala haitambuliki vya kutosha ukilinganisha na simulizi za mafanikio waliyofanya wanaume.

Kupitia chapisho hili mtasoma safari ya maisha ya uongozi mahiri wa Kibena Kingo Nassoro aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro (2010-2020); Mary Kunambi, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Kibuko-Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro (2015-2020); Anipher Kasimu Chiwile aliyekuwa Diwani wa Kata ya Makuburi katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Jijini Dar es salaam (2015-2020); Ndeshukurwa Akyoo Tungaraza, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Makongo katika Halmshauri ya Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es salaam (2015-2020); na Helgatiel Mchomvu aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmshauri Hai na Diwani wa kata ya Muungano mkoani Kilimanjaro (2015-2020).

Kestoria hizi za kiragbishi zinatupa mafunzo mengi kama vile umuhimu wa vyama vya siasa kuweka mazingira wezeshi ya ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi, umuhimu wa taasisi za Serikali kuelekeza vyama vya siasa kutekeleza sheria zinazohusu usawa wa jinsia katika nafasi za maamuzi hususan sheria ya vyama vya siasa Tanzania ya mwaka 1992 iliyorekebishwa mwaka 2018; na ushiriki wa jamii katika kuondoa mila, desturi na mifumo kandamizi inayokwamisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi na uongozi.

Wakati ukifungua kurasa mbalimbali za kitabu hiki, utajumuika nasi katika kutambua na kusherekea maisha ya uongozi wa wanawake uliosheheni mikakati na mbinu mbalimbali za kutatua changamoto za kijamii na michango yao katika maendeleo ya jamii na taifa. Kitabu hiki ni fursa kwa wanawake, mashirika yanayotetea haki za wanawake na usawa wa jinsia, vyama vya siasa na watunga sera ambao nao wote wanahusika katika harakati za kuleta usawa wa kijinsia katika nchi yetu na duniani kwa ujumla kujifunza mikakati mbali mbali waliyotumia hao viongozi mahiri, mafanikio yao, changamoto walizokutana nazo na jinsi walivyokabiliana nazo.

Kupitia simulizi hizi zenye kutoa picha halisi, ni matumaini yangu kuwa kitabu hiki kitachokoza na kuchochea mjadala mpana katika jamii ili kubadili mitizamo hasi dhidi ya wanawake na kuwa na picha sahihi ya michango ya wanawake katika maendeleo ya taifa letu.

Nakutakia usomaji mwema wenye furaha.

Lilian Liundi
Mkurugenzi Mtendaji

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)

Utangulizi

TGNP tangu kuanzishwa kwake ilitambua kwamba ili kujenga jamii na taifa linalozingatia usawa wa kijinsia na haki za wanawake ni lazima kuwa na ushiriki wa wanawake na makundi mengine katika jamii katika mchakato wa kutoa maamuzi na nafasi za uongozi katika nyanja zote kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika kufikia azma hiyo, TGNP imekuwa ikifanya kazi na wadau mbalimbali zikiwemo asasi za kiraia, Serikali, wadau wa maendeleo, na taasisi binafsi katika kufanya ushawishi, uchechemuzi kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa uongozi katika nyanja mbalimbali, hususani nyanja ya siasa.

Tangu mwaka 1995, TGNP imekua ikiendesha mafunzo ya ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa ngazi ya Serikali za mitaa na Serikali kuu. Mafunzo hayo ni kwa ajili ya watiania, wagombea, viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa; kufanya ushawishi kwa taasisi za Serikali zinazosimamia uchaguzi ili kuwezesha michakato ya uchaguzi kwa kufuata misingi ya usawa wa kijinsia. Mwaka 2000, TGNP kwa kushirikiana na asasi wanachama wa mtandao wa FEMACT ilianzisha kampeni ya hamsini kwa hamsini (50/50) katika ushiriki wa nafasi mbalimbali za maamuzi. Hii ilitokana na nchi yetu kuridhia mikataba na matamko ya kikanda na kimataifa kuhusu kuongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi. Kampeni hiyo iliambatana na kuandaliwa kwa ilani zilizobeba tamko la madai ya wanawake katika uchaguzi; muendelezo wa mafunzo mbalimbali, kujenga uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika uongozi; chambuzi mbalimbali za muktadha wa kisiasa, kisera na kisheria pamoja na hali halisi ya ushiriki wa wanawake katika ngazi ya kisiasa na nini kifanyike na chambuzi hizo zilitumika katika uchechemuzi.

Kampeni hii ilichangia katika ongezeko la idadi ya wanawake viongozi katika ngazi ya kisiasa, mfano katika nafasi za ubunge, wanawake waliongezeka kutoka asilimia 11.2 mwaka 1995 hadi asilimia 39.6 mwaka 2020 kabla ya Uchaguzi Mkuu (IPU, 2020). Tumeshuhudia, katika historia ya Tanzania, tangu kupata uhuru kwa mara ya kwanza wagombea wanawake walijitokeza kugombea nafasi ya urais kutoka vyama mbalimbali; Anna Senkoro aligombea mwaka 2005 kupitia chama cha PPT Maendeleo, Anna Mghwira aligombea mwaka 2015 kupitia chama cha ACT Wazalendo, Queen Cathbert Sendinga aligombea mwaka 2020 kupitia chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) na Cecilia Augustino Mwanga aligombea mwaka 2020 kupitia chama cha Demokrasia Makini. Vile Vile, nchi yetu iliweka historia mpya ya kuwa na makamu wa Rais wa kwanza mwanamke Mh. Samia Suluhu Hassan na Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge la 10 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Anna Semamba Makinda.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi bado ni mdogo. Uwakilishi wa wanawake Wabunge na Madiwani

hususani wakuchaguliwa bado ni mdogo sana; wanawake ni asilimia 10 tu ya Wabunge 264 wakuchaguliwa na asilimia 5.2 tu ya Madiwani 3946 wa kuchaguliwa (NEC, 2016). Vile vile, nafasi za uteuzi bado ni changamoto hasa kwa wanawake. Mfano. Mawaziri wanawake ni asilimia 16.7 tu ya Mawaziri wote, na Makatibu Wakuu ni asilimia 18.5 tu. Takwimu zinaonesha bado kuna safari ndefu kuelekea usawa wa kijinsia, yaani 50/50 katika nafasi za maamuzi.

Wakati Tanzania ikielekea katika uchaguzi wa Serikali za mitaa (2019) na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi ni muhimu sana. Kwa kupitia michakato ya uongozi wa wanawake, TGNP ikishirikiana na washirika wake likiwemo shirika la maendeleo kutoka nchini Norway (Norad) inalenga kuchangia katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa kupitia uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. TGNP itaendelea kuimarisha tapo au nguvu za pamoja katika ukombozi wa wanawake kimapinduzi kwa kuhamasisha, kushawishi na uchechemuzi kuhusu umuhumu wa ushiriki wa wanawake katika shughuli za uongozi na katika nafasi mbalimbali kwenye ngazi za kijamii na kitaifa. Kwa kushirikiana na wadau wake, TGNP itaimarisha na kutekeleza mikakati yake ya kutambua viongozi wanawake vijana na watu wenye ulemavu wenye uwezo wa kuwa viongozi, na wale ambao tayari ni viongozi katika nyanja mbalimbali ili kuwashawishi waweze kutia nia katika nafasi mbalimbali kwenye chaguzi hizi. Vile vile itaendelea kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo watiania, wagombea; vyama vya siasa; wadau muhimu; taasisi za Serikali zinazosimamia uchaguzi na vyombo vya habari; kuandaa na kusambaza tamko la madai ya wanawake katika uchaguzi; kuandaa na kuendesha programu ya ukungwi/ulezi wa viongozi wanaochipukia; kuandaa vilinge vya simulizi za safari za uongozi kati ya viongozi wanawake mahiri waliobobea na wale wanaochipukia ili kushirikishana uzoefu na mbinu za ushindi katika uchaguzi; kuandaa simulizi/kestoria za wanawake mahiri katika uongozi wa kisiasa.

Kutokana na nguvu ya simulizi katika kuleta mabadilko katika jamii, TGNP iliona umuhimu wa kuandika kestoria za Madiwani mahiri wanawake wa mfano waliioonesha uwezo wao madhubuti wa kuongoza kwa ujasiri na walioshiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika kata zao na nje ya kata zao. Kestoria hizi za kiraghbishi zinaeleza safari ya wahesimihiwa Madiwani wanawake watano ambao ni; Kibena Kingo Nassoro aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro (2010-2020); Mary Kunambi, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Kibuko Mkoani Morogoro (2015-2020); Ndeshukurwa Akyoo Tungaraza, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Makongo katika Halmshauri ya Kinondoni Jijini Dar es salaam (2015-2020); Anipher Kasimu Chiwile aliyekuwa Diwani wa Kata ya Makuburi Jijini Dar es salaam (2015-2020); na Helgatiel Mchomvu aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmshauri Hai na Diwani wa kata ya Muungano mkoani Kilimanjaro (2015-2020).

Muktadha

Demokrasia, uwajibikaji na uongozi bora jumuishi ni vichocheo muhimu katika nyanja zote za maendeleo ya nchi ikiwemo kuimarika kwa upatikanaji wa haki za binadamu.

Taarifa za shirika la UN Women na IPU (2017) zimeonesha ongezeko dogo katika nafasi za uongozi katika Serikali na bunge, kidunia pamoja na Serikali mbalimbali kuridhia mikataba na matamko mbalimbali ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kwenye uongozi na nafasi za kisiasa tangu mwaka 1948 ziliporidhia Tamko la Haki za Binadamu.

Matamko kadhaa ya kimataifa na ya kikanda yameainisha haki za kiraia na kisiasa kwa wote bila ya kujali jinsi, rangi, au dini. Tamko la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu (1948) ambalo linachukuliwa kama msingi na muhimili mkuu kuhusu haki za kiraia na za kisiasa linatoa haki kwa kila mtu kushiriki katika utawala wa nchi. Azimio la Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Kisiasa (1966),vile vile linatoa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika kufurahia haki zao zote za kiraia na za kisiasa. Zaidi ya hayo, kanuni inayozuia ubaguzi katika haki za jinsia imeelezwa kwa umakini katika vyombo mbalimbali ikijumuisha Mkataba wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (1979); Azimio la Beijing la mwaka 1995 na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Azimio la Beijing; Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za wanawake (2003); Itifaki ya SADC ya Jinsia na Maendeleo (2008) na Mkataba wa Afrika juu ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (2007) unakusudia “kukuza usawa wa kijinsia, mchakato wa utawala na maendeleo”.

Mkutano wa nne wa Dunia wa Wanawake uliofanyika Beijing mnamo mwaka 1995, ulionesha kuendelea kutokuwepo kwa usawa kati ya wanaume na wanawake katika kufanya maamuzi. Mpango kazi wa Utekelezaji wa Azimio la Beijing lilisisitiza kwamba “ushiriki sawa wa wanawake katika kufanya maamuzi hauhitaji tu haki au demokrasia, bali ni lazima uonekane kama sharti muhimu ili maslahi ya wanawake yazingatiwe. Bila mtazamo wa wanawake katika ngazi zote za uongozi, malengo ya usawa, maendeleo na amani hayawezi kufikiwa”.

Nchini Tanzania kuna katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (77) ambapo ibara ya 12 (i,ii) inaonesha misingi ya usawa inavyotakiwa kutoa miongozo kwenye misingi ya sera na sheria zote ambazo zinahakikisha upatikanaji wa haki za binadamu; Ibara ya 21 (ii) ya katiba hiyo inasisitiza ushiriki wa wananchi katika masuala ya michakato ya utawala na uongozi. Kutokana na mabadiliko ya katiba yaliyofanyika 2014, ibara ya 66 (i) iliweka hatua za upendeleo (Affirmative action) za kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi, na kuonesha kuwa ushirikishwaji wa wanawake kwenye ubunge uwe si chini ya asilimia 30, jambo ambalo lilisaidia wanawake kuingia bungeni kwa kuchaguliwa majimboni, Viti Maalum na nafasi tano za uteuzi wa Rais.

Pamoja na kuwepo kwa hayo makubaliano na mikataba mbalimbali bado ushiriki wa wanawake katika uongozi wa kisiasa ni mdogo sana katika ngazi ya kidunia, kikanda na hata kitaifa hususani katika nafasi za kuteuliwa, utumishi wa umma, sekta binafsi au katika taaluma.

Wanawake bado wanaendelea kutengwa katika vyombo vya kufanya maamuzi duniani kote licha ya kuwepo kwa mifumo ya kawaida ya kutetea usawa wa kijinsia. Ukilinganisha na wanaume, wanawake bado wameendelea kuwa na uwakilishi mdogo katika nafasi za kuchanguliwa na za kuteuliwa. Takwimu[1] zinaonesha kuwa hadi Januari 2019, wanawake wakuu wa nchi (Head of state) walikuwa 10 kati ya 152 (asilimia 6.6) tu ambapo wanawake wakuu wa Serikali (head of government) walikuwa 10 kati ya 193 (asilimia 5.2). Kwa upande wa Afrika kwa sasa kumekuwa na Marais wanne wanawake, aliyekuwa Raisi wa Malawi, Joyce Hilda Banda (Aprili 2012- Mei 2014), aliyekuwa Raisi wa Liberia, Ellen Johnson Sirleaf (Januari 2006-Januari 2018), aliyekuwa Raisi wa Mauritius Ameenah Gurib-Fakim (Juni 2015- Machi 2018) na Raisi kutoka Ethiopia Sahle-Work Zewde (Oktoba 2018 hadi leo).

Vile vile takwimu zinaonesha kuwa hadi Januari 2019, kidunia maspika Wabunge wanawake ni asilimia 19.7 na manaibu spika wanawake ni asilimia 28.2. kulingana na ripoti hiyo hiyo, Wabunge wanawake katika nchi zote walikuwa ni asilimia 24.3. Pia kufikia Juni 2017 nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kulikuwa na wastani wa Wabunge wanawake asilimia 23.7.

Katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazofanya vizuri katika ushiriki wa wanawake katika uongozi. Kulingana na takwimu za Interparliamentary Union (IPU) hadi Januari 2019, Tanzania inashika nafasi ya pili kwa nchi za Afrika Mashariki na nafasi ya 25 duniani kwa kuwa na asilimia 36.9 ya wanawake Wabunge ambapo Rwanda imeshika nafasi ya kwanza hadi kidunia kwa kuwa na asilimia 61.3. Hata hivyo nchi yetu haijaweza bado hatujaweza kufikia 50/50 na hivyo, hatuna budi kuongeza juhudi katika kuongeza nafasi za wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi ili kufikia lengo hilo.

Kwa nchi ya Tanzania, kwa mara ya kwanza baaada ya uhuru imeweza kuwa na mwanamke wa kwanza kuwa Makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu Hassan mwaka 2015-2020. Vile vile, kwa mara ya kwanza katika kestoria ya Tanzania kumekuwa na Spika wa Bunge mwanamke Mh. Anne Semanga Makinda (2010-2015) katika Bunge la 10 ambaye alifuatiwa na Dr. Tulia Mwansasu Akson kama Makamu Spika wa Bunge la 11 (2015-2020). Kwa upande wa Wabunge wa kuchaguliwa, wanawake ni 25 kati ya Wabunge 264 wa kuchaguliwa ambayo ni sawa na asilimia 9.5 tu ya Wabunge wote; idadi ya Wabunge wanawake

1 Inter-parliamentary union report 2019

wa Viti Maalum ni 113 ambayo ni sawa na asilimia 29 ya Wabunge wote. Jumla ya Wabunge wanawake ni 142 sawa na asilimia 37 ya idadi ya Wabunge wote ambao ni 393. Hii bado ni idadi ndogo ukilinganisha na lengo la kufikia asilimia 50/50.

Uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa katika ngazi ya udiwani bado ni changamoto kubwa. Licha ya juhudi za wadau mbalimbali ambazo zinafanyika ikiwemo Serikali, AZAKI na wadau wa maendeleo. Takwimu zinaonesha kuwa (NEC, TEMCO) idadi ya Madiwani wanawake wa kuchaguiwa kutoka kwenye Kata ni 204 kati ya Madiwani wote 4285 ambao ni sawa na asilimia 5 ya Madiwani wote. Madiwani wanawake wa Viti Maalum ni 1,611 sawa na asilimia 30 ya Madiwani wote. Kwa ujumla wanawake Madiwani ni 1,815 sawa na asilimia 33.9 ya Madiwani wote. Madiwani wa kuchaguliwa ndio wenye fursa za kugombea na kushika nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ambalo lina mamlaka ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Halmashauri. Kwa bahati mbaya ushiriki mdogo wa wanawake Madiwani wa kuchaguliwa unawanyima wanawake wengi kushika nafasi za uenyekiti wa Halmashauri. Tanzania bara ina jumla ya Halmashauri 185 ambapo ni Halmashauri 6 tu sawa na asilimia 3.2 ambazo zinaongozwa na wanawake Wenyeviti.

Ikumbukwe kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wanaishi katika ngazi ya vijiji na kata na chimbuko la maendeleo ya nchi katika ngazi hiyo. Hivyo, ushiriki mdogo wa wanawake katika nafasi hizo muhimu na za kimkakati ni changamoto katika kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo jumuishi na endelevu.

Ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi na uongozi wa kisiasa unategemea sana utashi wa vyama vya siasa kwa sababu ndivyo lango kuu la kuingiza viongozi wa siasa madarakani katika nyanja zote. Hata hivyo, kati ya vyama vya siasa 19 vilivyosajiliwa ni chama kimoja tu chenye Mwenyekiti mwanamke sawa na asilimia 5.2 ya Wenyeviti wa vyama vyote (Julai 2020). Kwa upande wa watendaji wa kuu (Makatibu Wakuu), ni vyama vitatu tu sawa na asilimia 15.7 ambavyo Makatibu Wakuu wake ni wanawake. Kunahitajika juhudi za makusudi ndani ya vyama kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi. Vile vile, mamlaka husika za Serikali ziwajibishe vyama vya siasa kuhusu usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi ndani na nje ya chama kama sheria ya vyama vya siasa ilivyotamka usawa wa kijinsia kama msingi mmoja wapo wa katika sheria hiyo.

MH. KIBENA KINGO NASSORO

Diwani wa Kata ya Ngerengere na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini (2010-2020)

"Uongozi ni kuwatumikia watu na si kujinufaisha mwenyewe. Ili mtu kuwa kiongozi mzuri anapaswa kuwa mzalendo, mwenye weledi na umahiri katika kazi yake".

Wasifu

Mh. Kibena Kingo Nassoro ni mojawapo wanawake mahiri Wenyeviti watano tu wa Halmashauri 185 zilizopo Tanzania bara. Pia, Mh. Kibena ni Diwani wa kata ya Ngerengere. Ni mzaliwa na mkazi wa Kijiji cha Ngerengere wilaya ya Morogoro mkoani Morogoro. Alisoma katika shule za msingi Ngerengere na Bigwa wilayani Morogoro. Akiwa katika shule ya msingi Bingwa, Mh. Kibena alishika nafasi ya kiranja mkuu (dada mkuu) hadi alipomaliza darasa la saba shuleni hapo. Hakuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu kipindi hicho shule za sekondari za Serikali na za kulipia binafsi zilikuwa ni chache sana ukilinganisha na wahitimu. Badala yake, alifanya kazi kama Afisa wa Magereza katika gereza la Kihonda na baadaye kuhamishiwa katika kitengo cha kupokea simu kama mratibu wa simu za nje na ndani katika ofisi ya Magereza Mkoa wa Morogoro. Kazi hiyo aliweza kuifanya kwa umahiri mkubwa sana tangu akiwa Afisa Magereza. Wakati ajira za muda ziliposimamishwa, alienda kuhudhuria kozi ya mwaka mmoja katika Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii ya Bigwa. Baada ya kumaliza mafunzo yake ya maendeleo ya jamii, Mh. Kibena alitafuta msaada kutoka kwa baba yake kwa ajili ya mafunzo zaidi au kazi.

Kati ya mwaka 1984 na 1992, Mh. Kibena alifanya kazi kama Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Legeza Mwendo wilayani Morogoro na wakati huo huo alikuwa akifanya kazi kama Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya kata kwa kuwa kipindi hicho kulikuwa na chama kimoja tu. Kuanzia mwaka 1995 hadi 2000, alikuwa mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro anayewakilisha Vijana. Pia, alifanya kazi kama Katibu wa Umoja wa Vijana CCM wilaya za Morogoro na Kilombero mkoani Morogoro kati ya mwaka wa 1996 na 1998. Alipandishwa cheo na kushika nafasi ya Katibu wa vijana CCM mkoa wa Mtwara kati ya mwaka 2006 na 2008. Mwaka 2007 Mh. Kibena alijiunga na masomo ya QT ambapo mwaka 2008 alifanya mtihani wa kidato cha nne. Mh. Kibena aligombea na kushinda nafasi ya udiwani wa Kata ya Ngerengere katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na 2015.

Safari ya Uongozi wa Kisiasa

Baada ya kumaliza mafunzo yake ya maendeleo ya jamii, Mh. Kibena alirudi nyumbani na kupendekeza kwa baba yake apelekwe shule au amsadie kupata kazi. Namnukuu "*Nilikuwa king'ang'anizi kidogo! Nilianza kumsumbua baba yangu, Mzee Kingo Nasssoro Chambe ambaye kwa wakati huo alikuwa mtumishi wa umma. Nilimwambia kwamba nataka moja ya mambo haya mawili; aidha unanipeleka shule au unanisaidia kupata kazi. Kwa kipindi kile, mama yangu Bi Asha Saidi Mnyanga alikuwa mkulima na mjasiriamali katika kata ya Ngerengere.*".

Baba yake, ambaye kwa wakati huo alikuwa Mwenyekiti wa CCM kata Bingwa alichagua chaguo la pili na kumtafutia kazi kwa sababu kwa wakati huo ndio ilikuwa rahisi kwake. Aliajiriwa kama Katibu wa Tawi la CCM na Mtendaji wa Kijiji Legeza mwendo. "*Nilikuwa na umri wa miaka 19 wakati huo. Katika makuzi na uongozi wangu baba yangu alikuwa mfano mzuri na mlezi mwelekezi (role model& mentor) katika masuala ya uongozi. Katika nafasi yake ya uongozi baba alikuwa kimbilio la wale aliokuwa akiwaongoza ndani hadi nje ya eneo lake la uongozi. Alikuwa mzee maarufu sana na alitengeneza urafiki sana na watu. Mara nyingi alikuwa anatafuta suluhu ya matatizo na migogoro, amekuwa akiwa suluhilo na si tatizo katika jamii. Naamini hata kama sijafikia alipofikia baba, nimepiga hatua sana kuifuata nyao yake*".

Alifanya kazi katika nafasi hiyo katika kijiji cha Legeza Mwendo kutoka mwaka 1984 hadi 1992. "*Katika kipindi hiki najivunia kutokana na uongozi wangu tulifanikiwa kujenga shule ya msingi Mwenge ambapo niliisimamia toka msingi unapoanza kujengwa. kwa kushirikiana na wananchi tulifyatua matofali ya kuchoma na kukusanya mawe. Wanangu wote wawili walisoma katika shule hiyo.*" Bi Kibena alitoa mfano wa kazi nzuri aliyofanya akiwa Mtendaji wa kijiji. Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi mnamo 1992 na mgawanyo wa shughuli za Serikali na shughuli za chama, wafanyakazi walitakiwa kuchagua kati ya kufanyia kazi

Serikali au chama. Kutokana na ndoto yake ya kuwa kiongozi mkubwa wa kisiasa, Mh. Kibena alichagua kubaki katika chama na alipandishwa nafasi na kuwa Katibu wa Chama Kata ya Mkambarani wilayani Morogoro vijijini. Wakati akifanya kazi kama Katibu wa chama wa Kata, Mh. Kibena aliteuliwa kugombea nafasi ya Udiwani wa Viti Maalum anayewakilisha vijana na akashinda nafasi hiyo. Anasema, "*Kwanza umri wangu uliruhusu kuteuliwa katika nafasi hiyo na pili ni umahiri wangu katika kazi. Nilipigiwa kura na baraza la Madiwani, nilishindana na mgombea mwanaume na nikafanikiwa kumshinda baada ya kujieleza vema*".

Mwaka 1996, kutokana na utendaji wake mzuri wa kazi Mh. Kibena aliteuliwa kuwa Katibu wa Vijana wa Chama wa Wilaya Morogoro mjini. Mnamo mwaka wa 1998 alihamishiwa Morogoro vijijini katika nafasi hiyo hiyo hadi mwaka 2005 wakati alipohamishiwa wilaya ya Kilombero. Kwa kipindi chake chote cha uongozi Mh. Kibena alikuwa mfano katika utendaji kazi wake na ushirikano na wale anaowaongoza pamoja na vongozi wenzake. Alikwa kiongozi makini, mwenye hekima, mtulivu na msikivu asiye kuwa na papara katika kutoa maamuzi, hii ndio maana mnamo mwaka 2006, alipandishwa cheo na kuwa Katibu wa Vijana wa Chama wa Mkoa wa Mtwara. Katika nafasi hiyo alisimamia uanzishwaji wa matawi ya vijana vyuoni hususan Chuo Kikuu cha Sokoine, maarufu kama SUA na Chuo kikuu ha Mzumbe mkoani Morogoro. Mh. Kibena ni mfano halisi kwamba vijana wanawake wana uwezo mkubwa wa kuongoza wa kipewa nafasi.

Mwaka 2010 katika uchaguzi mkuu, Mh. Kibena aliamua kuingia katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi ya udiwani wa Kata ya Ngerengere na kuibuka kidedea kwa kishindo ndani ya chama dhidi ya wagombea wengine wanne wanaume na katika kata dhidi ya wagombea wawili wanaume wa vyama vya upinzani.

Mh. Kibena pia alijitokeza kugombea nafasi ya uenyekiti wa Halmashauri kati ya Madiwani wanawake watano wakuchaguliwa waliopo katika Halmashauri hiyo, aliweza kushinda dhidi ya wagombea wengine wawili wanaume kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti aliyekuwa anamaliza muda wake. Na hivyo, kuwa mwanamke wa kwanza Mwenyekiti katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini na mkoa wa Morogoro. Anaeleza, "*Viongozi wa chama changu katika ngazi ya wilaya hawakuniunga mkono wakati nagombea kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Walinitaka nigombee nafasi ya Naibu Mwenyekiti. Kuona hivyo, niliamua kukusanya fomu za nafasi ya Mwenyekiti na nafasi za Naibu Mwenyekiti. Kwa mshangao wa watu wengi, siku ya kurudisha fomu za uteuzi nilirudisha tu fomu kwa ajili ya nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri. wagombea wengine walikuwa wakishawishi wateuliwe lakini sikuwahi kushawishi jina langu lipate kuteuliwa. Nilikuwa na uhakika kuwa rekodi yangu nzuri kwenye chama ilikuwa inatosha. Ninamshukuru Mungu jina langu liliteuliwa pamoja na majina mengine mawili*".

Mh. Kibena alikabiliwa na upinzani mkali na wakati mwingine upinzani uliotoka moja kwa moja kwa viongozi wake. Vile vile, katika michakato ya uteuzi, mara nyingine wale ambao hawajateuliwa huungana na wapinzani wako ili kuhakikisha kuwa unashindwa. Hili lilijitokeza kwa Mh. Kibena pia. Licha ya mashindano na upinzani mkali, Mh. Kibena alishinda uchaguzi huo na kutumikia kama Mwenyekiti wa Halmashauri kwa miaka mitano kutoka mwaka 2010 hadi 2015.

Katika kipindi chake cha kwanza cha uenyekiti, Mh. Kibena alionesha umahiri wake katika kuendesha vikao vya Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo. Kusema ukweli, Madiwani wengi walikuwa wanaukubali uongozi wa Mh. Kibena kutokana na kujituma, kujitoa, hekima, busara na utulivu katika kufanya maamuzi. " *Kwa kipindi kile tulifanikiwa kujenga ofisi za kata zote na vyombo vya usafiri na masoko makubwa kwenye tarafa tatu ambazo ni Mkuyuni, Matombo na Ngerengere. Nilifanya hivyo kwa mapato ya ndani. Najivuna tulijenga zahanati saba katika vijiji vya Lubungo, Matehim, Kichangani, Dakawa, Singisa, Selembala, na pia tulisimamia ufunguzi wa barabara mbalimbali katika kata yetu".*

Mnamo mwaka 2015, Mh. Kibena aliamua kugombea tena katika uchaguzi mkuu. Tofauti na ilivyokuwa mwaka 2010, kipindi hiki kazi haikuwa ngumu sana kwa sababu ya uwezo wake wa kuongoza, mchango wake kwa wananchi anaowatumikia na ushirikiano wake na viongozi wenzake. Mh. Kibena alipambana na wanaume wanne katika uteuzi ndani ya chama na akaibuka kidedea. Anaeleza "*Nilishinda kwa kishindo kwa kura 886 na wagombea wengine wote walipata kura 230. Ninaweza kukuhakikishia kuwa nilichaguliwa kwa sababu ya upendo wa watu na pia umahiri wangu katika kazi; sijawahi kutumia pesa kwa kweli mimi kwenye suala ya kazi sina utani wala mchezo. Kuanzia hapo tukaingia katika uchaguzi mkuu halisi. Mwishowe, nilishinda katika vituo vyote vya kupiga kura isipokuwa kimoja. Ama kwa hakika mchakato wa uchaguzi ni kama vita ili ushinde inategemea umejipanga vipi kumshinda adui yako.*"

Waswahili husema safari moja uanzisha nyingine, baada ya kushinda uchaguzi Mh. Kibena alianza safari yake ya kuongoza Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Morogoro kwa mara nyingine. "*Kama nilivyosema hapo awali, wakati mwingine viongozi wenzako wanaweza kukukatisha tamaa au hata kuungana na wapinzani wako usishinde. Kuna baadhi ya viongozi katika baraza hawakupenda mimi niwe mwenyekiti japo hawakuonesha wazi. Kwa mshangao wao, nilipata kura za uteuzi wa vyama za kutosha na kuendelea kushinda nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri".*

Kujenga Ujuzi na Ustadi wa Uongozi

Tangu mwaka 2009, Mh. Kibena alikuwa akihudhuria mafunzo, semina na mikutano inayoandaliwa na TGNP ambayo ilichangia kuongeza ustadi wake wa uongozi wa kisiasa. "*Mafunzo ya awali yalilenga kujenga uwezo wetu kama wanawake kuingia katika nafasi za kuchaguliwa. Kwa wakati huo nilikuwa Diwani wa Viti Maalum lakini nilipanga kugombea nafasi ya Diwani wa kata wa kuchaguliwa. Nilijifunza ujuzi mwingi wa kampeni ambao niliutumia na kushinda uchaguzi. Tangu wakati huo, TGNP imeendelea kujenga uwezo wetu kwa mfano katika kuandaa bajeti zinazozingatia usawa wa jinsia. Fursa nyingine ambao niliipata kupitia TGNP ni ile ya ziara za kujifunza na kushirikishana uzoefu na Madiwani wa kata mbalimbali hususani zile zenye Vituo vya Taarifa na Maarifa kuona jinsi wananchi wanavyoshirikiana na viongozi katika kuleta Maendeleo. Elimu tuliyoipata katika ziara hizi ziliisaidia manispaa ya Morogoro kwa mara ya kwanza (2018/2019) kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa taulo za kike katika shule za umma. Nimekuwa nikipigania hiyo sio tu katika baraza langu lakini pia mikutano mingine kama Jumuiya za Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) katika ngazi ya mkoa na kitaifa. Ninapokuwa kwenye mikutano wenzangu wanasema kuwa mwanaharakati huyu wa kike anataka kutuondoa katika nafasi zetu ukizingatia Wenyeviti wengi wa Halmashauri ni wanaume".*

Mnamo mwaka 2014, Mh. Kibena pia alihudhuria mafunzo ya uongozi yaliyofanywa na Taasisi ya ICLD jijini Nairobi. Alihudhuria pia awamu ya pili ya mafunzo ambayo yalikuwa nchini Uswidi na awamu ya tatu huko Afrika Kusini. "*Awamu ya mwisho ilifanywa mjini Morogoro mnamo 2015 baada ya kuombwa kuwa mwenyeji wa mafunzo. Mafunzo haya yameongeza uelewa wangu sana na kupanua uwezo wangu. Mafunzo yalikuwa kwenye utawala bora, uwezo wa kujadili na kutekeleza maamuzi; na kusimamia ustawi wa baraza".*

Mh. Kibena pia anatathmini fursa zake za hapo awali za kufanya kazi kama Katibu wa chama wa tawi na kama Afisa Mtendaji wa kijiji na uwezo ulipatikana hapo. "*Uzoefu kama huu uliniwezesha kukuza ujuzi na kunipa uwezo wa kusimamia na kutoa hoja. Nina uwezo wa kusimamia na kuongea hata katika mikutano ya kimataifa. ICLD hunialika mara nyingi; hata hapa nchini mashirika mengi yasiyo ya kiserikali hususan TGNP yamekuwa yakinialika ili kuwasilisha mada kwenye makongamano mbalimbali hata katika mikutano mbalimbali inayohusisha baadhi ya Wabunge na viongozi mbalimbali wa wizara, taasisi za umma na mashirika yasiyo ya kiserikali. Lakini pia, umuhimu wa kuwa karibu na watu; kwenye Serikali za mitaa kama hauko karibu na watu huwezi kuwaongoza na kuwasimamia vizuri".*

Mh. Kibena pia alipata maarifa na ujuzi wa uongozi kwa kusoma vitabu kuhusu siasa na uongozi na kujifunza kutoka kwa viongozi wa wanawake wa mfano. Anasema, "*Nimesoma vitabu vingi juu ya siasa na uongozi. Hata hivyo, ninavyopenda zaidi ni vya J. K. Nyerere vya Ujamaa na Kujitegemea, Uhuru ni Kazi, Muongozo wa CCM. Nimejifunza pia kutoka kwa viongozi wangu wanawake wa Tanzania*

wanaonipa hamasa kama vile Mh. Samia Suluhu Hassan, Mh. Anna Abdallah, Mh. Anna Makinda, Mh. Julie Maning na Mh. Getrude Mongela. Nimekuwa nikijaribu kujifunza na kuiga mitindo ya uongozi ya hawa viongozi mahiri wanawake".

Mh. Kibena ameweza kuimarisha mahusiano mazuri kati ya viongozi wa kisiasa na wataalam/ wafanyakazi wa baraza tofauti na mabaraza mengine nchini. "*Tangu nimekuwa Mwenyekiti hatujawahi kugawanyika na ninajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuelewa na kutumia kanuni na taratibu za kutatua migogoro yoyote inayoweza kujitokeza katika baraza.*' Mbinu hii ilimsaidia Mh. Kibena kuepuka/ kuepusha baraza kuingia katika migogoro katika kipindi chake cha uongozi.

Mafanikio katika Utekelezaji wa Ahadi za Uchaguzi

Ajenda kuu za Mh. Kibena zilitokana na uchambuzi yakinifu wa hali halisi ya changamoto katika wilaya ya ya Morogoro na kutoka na vipaumbele ambavyo ni kuongeza mapato ya baraza, kuboresha utoaji wa elimu, kuboresha huduma za afya, kuboresha miundombinu ya uchukuzi hususan barabara na pia kujenga fursa za ajira kwa vijana. Ameweza kutekeleza ahadi hizo kwa mafanikio mbalimbali.

Ajenda ya 1: Mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Wilaya

Mh. Kibena aliripoti kwamba wakati akiwania nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri, aliahidi kushirikiana na Madiwani wote na wataalam kupanga mikakati ya kuongeza mapato ya ndani. Anakumbuka jinsi alivyoongoza wataalam kutambua vyanzo vipya vya mapato na kuwashirikisha Madiwani kuhusu ufuatiliaji mzuri wa ukusanyaji wa mapato, mkakati ambao hatimaye ulizaa matunda mazuri. Anakumbuka, "*Mkakati wetu ulifanya kazi na kusababisha kuongezeka kwa mapato ya ndani kutoka milioni 500 hadi bilioni 2.3 kila mwaka. Kwa pesa hii, tulijenga masoko, madarasa na zahanati. Tumedhamiria kuendelea kuwa wabunifu katika kutambua na kushughulikia fursa zote ambazo zitaongeza mapato ya baraza. Nina hakika mapema au baadaye tutazidi rekodi yetu hii ya bilioni 2.3 kwa mwaka*".

Ajenda ya 2: Huduma za Afya

"*Niliposhika wadhifa huu, kulikuwa na zahanati 43 na vituo vya afya vitatu katika wilaya hii kubwa. Kwa kujitoa na kufanya kazi kwa bidii, sasa tuna zahanati 63 za Serikali, tumeboresha huduma katika vituo vyetu vitatu vya afya, tumejenga vyumba vya upasuaji, tulipata kwa kushirikana na wadau wa alliance club sweeden mashine ya ultra sound na kuanzisha huduma za damu salama katika vituo vyote vya afya wilayani. Mbali na hayo, vituo vitano (5) vipya vya afya vimekamilika na kimoja ndo kinaendelea kujengwa pamoja na hospitali ya wilaya chini ya mpango wa Rais wa kuboresha huduma za afya nchini*". Anafafanua Kibena.

Ajenda ya 3: Ajira kwa Vijana

Mh. Kibena yupo makini katika kushughulikia ukosefu wa ajira kwa vijana na kwa hivyo aliongoza Baraza katika kuanzisha na kutekeleza miradi kwa lengo hilo. "*Ajira ya vijana ni ajenda yetu muhimu.Tumewekeza katika miradi ya maendeleo ya sekta ya utalii huko kata za Kisaki na Bwakila Chini kupitia maporomoko ya maji Kinole na Maji Moto Kisaki. Tumetoa maghala ya kuifadhia chakula kwa vijana wa Bwakila Chini ili kuwawezesha vijana hao kuongeza thamani ya mazao watakayozalisha. Kusudi ni kuongeza mapato ya baraza na wakati huo huo kutoa fursa kwa vijana kupata ajira na kipato*".

Fursa zingine za ajira kwa vijana zinaonekana kwenye sekta ya kilimo. Mh. Kibena anafafanua kuwa "*Baraza limetenga ardhi ya kutosha ya uwekezaji katika kilimo. Wakulima wote wakubwa na wadogo wamekaribishwa kuwekeza. Hivi sasa, kuna wakulima ambao wamechukua hekta 16,000 katika bonde la Ukutui kulima miwa ya sukari na kuendesha kiwanda cha kusindika sukari kampuni inaitwa Morogoro Sugar. Pia, taasisi mbili za mfuko wa pensheni zimechukua ardhi ya kupanda miwa na kiwanda Mkulazi One. Wengine wamejenga kiwanda cha usindikaji wa mazao kama mbaazi huko Mkambarani. Kwa uwekezaji huu, vijana wetu watapata ajira*".

Ajenda ya 4: Miundombinu ya Usafirishaji

Kwenye ajenda ya kuboresha miundombinu ya uchukuzi, Mh. Kibena anasema "*Jiografia ya wilaya yetu ina changamoto sana. Ni ya mlima sana, na maeneo mengine ya mbali ni ya milimani mno kufikiwa na magari au pikipiki. Kusababisha uhaba wa watumishi katika baadhi ya huduma. Hata hivyo, tumeazimia kuboresha miundombinu katika wilaya hii. Ujenzi wa barabara ya Singisa (22km) inaitwa Senega Lumba Chini unaendelea na ukikamilika, utaboresha sana kuiunganisha wilaya*".

Utekelezaji wa Ahadi katika Ngazi ya Kata.

Mh. Kibena pia amejitahidi kutekeleza ilani zilizotolewa katika kata yake ya Ngerengere. Anaripoti juu ya mafanikio katika sekta ya afya: "*Kata yangu ina vijiji vinne na karibu watu 11,000 kwa sensa ya mwaka 2012. Tulikuwa na kituo kimoja cha afya wakati nachaguliwa lakini hakikuwa kinatoa huduma za upasuaji. Namshukuru Mungu sasa tumeibadilisha; tuna jengo la upasuaji, Ultra Sound na huduma ya Damu Salama na Afya ya Kinywa. Kama kiongozi Mwanamke najivunia mafanikio haya kwa sababu waliokuwa wanaathirika zaidi kwa kukosa huduma hizo ni wanawake na watoto. Pia tumeweza kujenga zahanati katika kijiji cha Kiwege ambayo haikuwepo wakati nachaguliwa kuwa Diwani;*". Juhudu hizi kwa kiwango kikubwa zimepunguza vifo vya uzazi kwani kwa sasa huduma za upasuaji, ultra sound na damu salama ni muhimu sana kwa wanawake wajawazito.

Kuhusu mafanikio katika sekta ya elimu, anasema: "*Pia tulikuwa na shule ya sekondari ya Ngerengere ya kutwa ambayo ilikuwa katika hali mbaya sana. Ilikuwa na vyumba vya madarasa nane. Sasa imeboreshwa na kuwa na vyumba vipya vya madarasa kumi na sita na kukarabati yale madarasa ya zamani nane. Tumejenga mabweni mawili. Ujenzi wa mabweni utasaidia kupunguza changamoto kutembea umbali mrefu na mimba za utotoni kwa watoto wa kike na kwa upande mwingine itaongeza ufaulu wa watoto wote hususan wa kike. Lengo letu ni kuifanya iwe shule ya sekondari hadi kidato cha sita na ujenzi wa madarasa unaendelea* ".

Kibena anaongeza "*Kuna kijiji kiitwacho Sinyaulime ambacho hakikuwa na shule ya msingi sasa kina shule na wanafunzi wanasoma kutoka darasa la kwanza hadi la saba. Barabara ya kwenda kijijini imeboreshwa na daraja la zamani la muda limebadilishwa na kuwekwa jipya na la kudumu. Pia tumeliboresha na kuliimarisha daraja la Ngerengere ambalo lilikuwa linaleta shida wakati wa mvua. Vilevile, tumejenga madarasa mapya sita katika shule za msingi za Kiwege na Njia nne kwa kushirikiana na wananchi*".

Mh. Kibena anafafanua juu ya ukweli kwamba miradi ya huduma za kijamii iliyotekelezwa katika kata yake ilitekelezwa kwa kutumia pesa zilizotengwa kupitia bajeti ya kawaida ya baraza na hakutumia nafasi yake kama Mwenyekiti wa Halmashauri ili kuleta maendeleo katika kata yake.

Changamoto na Mipango ya Baadaye

Changamoto nyingi ambazo Mh. Kibena amekutana nazo zinahusishwa na tabia ya siasa mbaya na unyanyasaji wa kijinsia. Anakumbuka juu ya matukio kadhaa ambayo washindani wake walimtuhumu kwa kutumia ujana wake kushinda nafasi za kisiasa. "*Mara ya kwanza ilikuwa mwaka 1998 wakati nilikuwa nagombea kuwa Mwenyekiti wa Vijana wa mkoa na baadaye nilipogombea Kiti Maalum cha Madiwani kupitia vijana. Nilishangaa sana kwa sababu sikuwepo wakati kamati*

ilipokuwa ikiniteua kugombea kuwa Mwenyekiti wa vijana katika ngazi ya mkoa. Lakini wapinzani wangu wa kiume walidai kuwa sikuchaguliwa kwa ubora lakini kwa sababu ya rushwa ya ngono. Inaumiza kusikia madai kama haya yasiyokuwa na msingi ya wanaume walioshindwa uchaguzi. Kawaida huwa napuuzia kwa sababu hizo ni siasa mbaya ambazo zinaweza kukutoa nje ya mpango wako wa kutimiza ahadi". Mh. Kibena ni mmojawapo wa viongozi wengi wanawake wanaokutana na changamoto ya dhana potofu iliyopo katika jamii kuwa nafasi wanazoshikilia zimetokana na rushwa ya ngono. Elimu zaidi kwa umma inahitajika ili kutokomeza dhana hizo na kwa upande mwingine, viongozi wanawake wanaotuhumiwa hivyo wanapaswa kuvunja ukimya na kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya hao wanao watuhumu.

Changamoto nyingine iliyokuja kama tishio ni ya mwaka 2012 wakati wanavunja mikataba ya ajira ya wafanyakazi 12 kwa sababu ya utovu wa nidhamu. "*Siku ya mkutano wa baraza, nilipokea ujumbe wa maandishi kwamba watu wawili walikuwa wanakuja na mabomu kulipua chumba cha baraza. Niliamua kushauriana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED) na nikamwambia aimarishe usalama katika eneo la baraza na kuhakikisha hakuna mtu mwingine anayejua kuhusu ujumbe huo. Tulifanya kikao na kuamua kuwafukuza wafanyakazi hao. Siku hiyo niliogopa sana, watu wengine walinifuata nyumbani kwangu kwa hivyo niliamua kutolala hapo kwa muda*". Licha ya kutishiwa usalama wake Mh. Kibena amekuwa jasiri katika kuwawajibisha watendaji ambao walikuwa hawatumii nafasi zao vizuri. Hilo ni funzo kwa viongozi wengine kutokuogopa kusimamia maamuzi ya uwajibikaji kwa kuogopa kutishiwa.

Mh. Kibena tayari ametoa uamuzi wake juu ya hatua yake inayofuata katika safari ya kisiasa. "*Nimeamua kustaafu siasa na kuwapa nafasi watu wengine wenye uwezo wa kuongoza. Hata hivyo, watu katika kata yangu na hata kwenye baraza wananiambia niutafakari tena uamuzi wangu. Sijioni nikibadilisha uamuzi huu. Nitaendelea kuushikilia. Ninaamini katika hekima ya zamani ya kustaafu wakati bado unapendwa*".

Kuwaandaa Viongozi wa Wanawake wa Baadaye

Mh. Kibena anaona kwamba, "*uongozi ni kuwatumikia watu na si kujinufaisha mwenyewe, ili mtu kuwa kiongozi mzuri anapaswa kuwa mzalendo. Zamani kulikuwa na vyuo vilivyotoa mafunzo katika siasa na uongozi. Mtu lazima awe tayari kuwa mzalendo. Ninachokiona siku hizi, vijana wengi wanakosa uzalendo. Kwa mfano, mtu akiteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Mkuu wa Wilaya, anapaswa kupatiwa mafunzo ya elimu ya uraia na uadilifu ili kuimarisha uzalendo na uwajibikaji wake. Vile vile, ni wajibu wa viongozi wenyewe kutafuta maarifa kupitia njia mbalimbali ikiwa hawakupatiwa mafunzo hayo ya uongozi kabla ya kutekeleza majukumu yake kama kiongozi. Hii itamsaidia kuongeza weledi na umahiri katika*

kazi yake. Inasikitisha sana kwa kiongozi kutanguliza maslahi yake mbele badala ya maslahi ya wananchi au mamlaka iliyompa dhamana ya kuwatumikia."

Mh. Kibena amekuwa akiandaa viongozi wanawake wa baadaye na kuwajengea uwezo waliopo kwenye nafasi za uongozi. "*Kupitia Umoja wa Wanawake wa Serikali za Mitaa (WASEMI) nimekuwa nikihimiza wanawake wenzangu kugombea nafasi za udiwani wa Kata. Mungu akipenda katika uchaguzi ujao tunaweza kuongeza idadi ya wanawake Madiwani katika Kata. Tunavyo viti vingi vya Madiwani wanawake wa kuteuliwa na tunataka wahame kutoka hapo hadi kuwa Madiwani wa Kata. Pia tunawaambia kwamba kuwa Mwenyekiti wa baraza inawezekana. Tumefanya mkutano chini ya Mfuko wa Wanawake Tanzania kule Dodoma ili kujenga uwezo wa wanawake hususan katika sheria za uchaguzi na kushinda unyanyasaji wa kijinsia.".*

Wito.

Mh. Kibena anatoa wito kwa wanaotarajia kuwa kuwa viongozi na viongozi kuwa na uzalendo na uadilifu katika kutumikia wananchi/ mamlaka zilizowapa dhamana ili kuleta maendeleo. Kwa upande mwingine, anahimiza jamii kubadilika na kutambua uwezo wa mwanamke katika kuongoza badala ya kuamini kuwa wanawake wanakuwa viongozi kupitia kubebwa au upendeleo. Kwa upande wa viongozi wanawake, Mh. Kibena amehimiza viongozi hao kubeba ajenda na vipaumbele vya wanawake kwa kuwa kutatua changamoto hizo ni kuinufaisha jamii kwa ujumla. Kwa mfano upatikanaji wa maji hautamsaidia tu mwanamke ila wote wanawake na wanaume katika jamii watanufaika na huduma hiyo.

MH. MARY KUNAMBI

Diwani wa Kata ya Kibuko mkoani Morogoro (2015-2020)

"Maendeleo hayana dini, chama wala itikadi. Ni muhimu kumchagua mgombea kwa kuzingatia uwezo wa kuwaongoza ili kufikia malengo ya maendeleo."

Wasifu

Mh. Mary Kunambi ni Diwani wa kuchaguliwa wa kata ya Kibuko katika Halmashauri ya wilaya Morogoro. Alichaguliwa mwaka 2015 na ametumikia nafasi hii mpaka mwaka 2020. Mh. Mary ni mwanamke pekee kwenye nafasi ya Udiwani wa kuchaguliwa sawa na asilimia 6.3 ya Madiwani wa kuchaguliwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro yenye jumla ya Madiwani wa kuchaguliwa 29. Halmashauri hii ina Viti Maalum 10 sawa na asilimia 31.3. Kwa ujumla Halmashauri ina jumla ya Madiwani 39.

Mh. Mary alizaliwa katika kijiji cha Mwalazi wilayani Morogoro vijijini. Mwaka 1982 alimaliza shule ya msingi Mwembe Songo ipo katika kata ya Mji Mpya Manispaa ya Morogoro. Wakati akiwa shule ya msingi, Mh. Mary alikuwa kiranja toka darasa la tano hadi la saba. Mwaka 1986 alihitimu katika shule ya sekondari Kigurunyembe iliyopo katika kata ya Kingo. Alipata mafunzo ya uongozi katika Chuo cha Maendeleo ya Mwananchi Bigwa mwaka 1989-1990. Pia, alipata mafunzo ya miezi mitatu viongozi na chipukizi yaliyoliandaliwa na Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) mkoani.

Safari ya Uongozi wa Kisiasa

Mh. Mary aliipenda sana siasa tangu alipokuwa shule ya msingi "*Nilitokea kupenda masuala/shughuli za kisiasa tangu nilipokuwa shule ya msingi. Nilipenda sana masomo yanayohusiana na siasa na nilikuwa nikifanya vizuri sana katika masomo hayo. Lakini pia, nilipokuwa katika shule ya msingi nilijiunga na chipukizi wa CCM mwaka 1978. Nilipenda kucheza halaiki na gwaride na pia kuimba nyimbo za kusifu nchi yetu na viongozi* ".

Alipomaliza masomo yake ya kidato cha nne, mwaka 1987 kulikuwa na uchaguzi ndani ya chama, ambapo aligombea ujumbe la baraza la UVCCM wilaya ya Morogoro na kushinda dhidi wagombea 15. Aliongoza katika nafasi hiyo hadi mwaka 1992. Aliendelea kugombea na kushinda nafasi hiyo hiyo katika ngazi ya kitaifa mwaka 1997 ambapo aliongoza hadi mwaka 2002.

Mnamo mwaka 2010 Mh. Mary aliteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum na alitumikia wadhifa huo hadi mwaka 2015. Anaeleza, " *Katika nafasi ya Viti Maalum, nilitetea maslahi ya wanawake. Nakumbuka kwa kushirikiana na Madiwani wengine, nilisimama kidete kuhakikisha kuwa milioni 30 za Halmashauri ambazo zilitakiwa kupelekwa kwingine zinabaki kwa ajili ya kuboresha zahanati kama ilivyokuwa imepangwa. Tulifanikiwa kujenga zahanati hiyo na wananchi wanapata huduma katika zahanati hiyo ambayo kwa sasa imepandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya".* Hata hivyo, Mh. Mary hakupendelea sana kutumikia kama Diwani Viti Maalum kwa kuwa nafasi hiyo ilionekana ya upendeleo. Hatimaye, aliamua kugombea udiwani wa kuchaguliwa.

Mwaka 2015 alipogombea na kushinda nafasi ya Diwani wa kata ya Kibuko dhidi ya wanaume watatu. Anaelezea kuwa uzoefu wake wa kufanya kazi kama Diwani wa Viti Maalum ulichochea uamuzi wake wa kugombea udiwani wa Kata. Anaelezea: "*Wakati naingia katika baraza kupitia Viti Maalum ilinisaidia kuelewa shida na changamoto mbali mbali zinazowakabili watu na jinsi ya kupigania haki zao katika mikutano ya baraza. Hiyo ilinitia moyo sana katika uamuzi wangu wa kugombea moja kwa moja kupitia kata badala ya kuwawakilisha wanawake kupitia Viti Maalum".*

Katika kura za uteuzi wa chama, Mh. Kunambi alishindana dhidi ya wagombea wengine watatu wa kiume. Anakumbuka kuwa ulikuwa ni ushindani mkali sana. "*Wagombea wengine watatu waliungana na kusema mwanamke hawezi kushinda. Walishirikiana na kupambana vikali ili kunishinda. Nami pia nilipambana kivyangu. Niliibuka mshindi na kupata uteuzi wa CCM".*

Kunambi anaeleza kwamba kulikuwa na mchuano mkali dhidi ya wanaume wengi waliokuwa na mtazamo hasi wa kijinsia, pamoja na wale waliotoka vyama vya upinzani. "*Wanaume wengi walitumia vitabu vya dini ili kupinga uwezo wangu wa kushika nafasi ya uongozi. Kwa mfano, walisema kwamba haijaandikwa katika vitabu vya dini kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi na kwa hivyo sikustahili kuwa kiongozi kwa kuwa ni mwanamke* ".

Mh. Kunambi anaripoti kwamba alilazimika kuomba hekima za baadhi ya viongozi wa dini wa eneo hilo ili kupinga hoja zinazotolewa na washindani wake. "*Nilimwendea kiongozi mmoja wa dini wa eneo hilo na kumuomba afundishe watu juu ya mafundisho sahihi ya uongozi wa wanawake. Kiongozi huyo alikubali na katika mahubiri yake alifundisha kuwa maendeleo hayana dini, chama wala itikadi na kwamba ni muhimu kumchagua mgombea ambaye alikuwa na uwezo wa kuwaongoza ili kufikia malengo yao ya maendeleo bila kujali dini au jinsi ya mgombea huyo mafundisho hayo yalibadilisha mazingira ya kampeni na yalinisaidia sana*".

Mh. Kunambi anakiri kwamba kazi ya kiongozi huyo wa dini ilileta tofauti na akaona ni rahisi kuzungumza na watu wakati wa kampeni. Alitumia pia maneno ya busara ya mwalimu J.K Nyerere ambaye alipinga aina zote za ubaguzi katika nchi yetu na kwamba yeyote atakayejaribu kuleta ubaguzi anapaswa kuogopwa kama ugonjwa wa ukoma. Mwishowe, aliibuka mshindi wa nafasi ya Diwani wa kata ya Kibuko. Changamoto aliyoipata Mh. Kunambi inatufundisha umuhimu wa kushirikisha viongozi wa dini katika kuhamasisha jamii umuhimu wa kuchagua viongozi kwa kigezo cha uwezo na si dini au jinsi. Viongozi wa dini wana waumini au wafuasi wengi na wanaaminika chochote watakachokisema kitaaminiwa na kutekelezwa.

Kujenga Ujuzi na Ustadi wa Uongozi

Katika safari yake ya uongozi, Mh. Kunambi amehudhuria mafunzo kadhaa ya kumjengea uwezo wa uongozi ambayo yameongeza maarifa na ustadi wa uongozi wake. Anaangazia, haswa umuhimu wa mafunzo na semina zinazotolewa TGNP, "*Mwanzoni, wakati nikiwa Diwani wa Viti Maalum, niliogopa kugombea nafasi ya udiwani wa kata lakini mafunzo ya TGNP yalinipa ujasiri. Vile vile, nilipata fursa ya kushiriki katika ziara za Madiwani kujifunza na kushirikishana uzoefu wa uongozi na namna ya kushirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo. Ziara hii ilinisaidia katika kuimarisha uelewa wangu wa uongozi na jinsi bora ya kushirikiana na wananchi hususan Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kibuko kuleta mabadiliko katika jamii yetu. Majukwaa mengine yaliyoweza kunijengea uwezo wangu wa uongozi ni pamoja na Tamasha la Jinsia ngazi ya wilaya na taifa ambalo huandaliwa na TGNP na kuleta pamoja wanaharakati na wadau mbalimbali wa maendeleo kusherekea mafanikio yaliyopatikana katika kuleta usawa wa kijinsia nchini, kutafakari changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo katika ngazi mbalimbali ikiwemo kwenye jamii tunazotoka".*

Kazi ya uongozi wa kisiasa wa Mh. Kunambi imetiwa chachu na viongozi wakubwa wanawake haswa Mh. Getrude Mongela na Mh. Anna Makinda. Mh. Kunambi anadai kwamba amejifunza kutoka kwa viongozi hawa wanawake wakubwa juu ya umuhimu wa kusikiliza na kutilia maanani mawazo ya watu wa kawaida na kuongoza kwa uadilifu. Mh. Kunambi anajiona kama kiongozi ambaye ni msikilizaji mkubwa na anayeongoza kwa uadilifu mkubwa.

Mafanikio ya Utekelezaji wa Ahadi za Uchaguzi

Ajenda ya 1: Sekta ya Afya

Kuboresha huduma ya afya ilikuwa ajenda kuu ya Mh. Kunambi. Anakumbuka "*Ajenda yangu kubwa ilikuwa ni kuboresha huduma za afya kwa sababu katika vijiji vyote vitatu vya kata hatukuwa na zahanati. Sasa tunajenga zahanati. Wakina mama walikuwa wanatembea umbali wa kilomita nane kupata huduma za afya, walijifungua njiani na wengine wamefariki njiani. Kutokana na adha hiyo, wanawake wengi walikuwa wanajifungulia nyumbani. Nilihamasisha wananchi kujitolea tofali, mawe na mchanga ili kujenga zahanati. Zahanati imeshaezekwa na Halmashauri wataleta hela ya kumalizia. Ujenzi huo umefikia kiwango cha kuezeka na Mh. Mbunge ameniahidi kunipa mabati mia moja. Ninaamini kwa muda mfupi ujenzi utakamilika na huduma zitapatikana kwa watu*".

Ajenda ya 2: Sekta ya Elimu

Ajenda nyingine ilikuwa inahusu kujenga shule ya sekondari ya Kibuko. Mh. Kunambi anafafanua kuwa "*Sehemu ngumu zaidi ilikuwa ni kutafuta na kupata eneo la ujenzi. Tumeweza kufanikiwa na watu wameahidi kuchangia ujenzi huo. Utaratibu ulicheleweshwa kwa sababu kijiji kimojawapo kilitaka kuhama kutoka katika kata hii lakini sasa mzozo umetatuliwa baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019. Tumekubaliana na Baraza la Maendeleo la Kata (BMK) kuanza uhamasishaji wa kutafuta rasilimali kuanzia Januari 2020 na natumaini kwa muda mfupi ujenzi utaanza na Serikali itatusaidia. Kwa hivi sasa wanafunzi wanasoma katika kata mama ya Mbuyuni.*".

Mh. Kunambi anaongeza kuwa, "*masuala mengine ya elimu niliyoweza kufanya kwa kushirikiana na viongozi wenzangu na wananchi ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya waalimu katika kijiji cha Mwaradhi; kuongeza vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Mwaradhi, vyumba vitatu katika shule ya msingi Kibungo chini, na kujenga matundu nane ya choo katika shule ya msingi Kibuko.*"

Ajenda ya 3: VICOBA

Mh. Kunambi pia aliahidi kushirikiana na wanawake katika kuimarisha vikundi vyao vya ujasiriamali ili waweze kuunda vikundi vya kuweka na kukopa fedha (VICOBA). Anaeleza kuwa "*Katika vijiji vyote vitatu wanawake wamehamasishwa na kuanzisha vikundi vya VICOBA. Mpaka sasa kuna vikundi saba vya wanawake vya VICOBA katika kata yangu jumla ya wanachama 140. Katika kijiji cha Mwalazi, wanawake wameanzisha mradi wa uzalishaji wa kokoto na wanauza na kupata kipato. Tumeiomba Serikali itupatie mashine ili kokoto ziweze kuzalishwa kwa viwango vinavyotakiwa*". Anaendelea kusema, *"Vikundi vimekuwa ni chachu ya kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Wanawake wengi kutoka kwenye vikundi hivyo walijitokeza kugombea katika nafasi za ujumbe wa Baraza la Kijiji wakati wa uchaguzi mkuu wa Serikali ya mitaa mwaka 2019.*"

Ajenda ya 4: Kupima na Kuhalalisha Ardhi

Mh. Kunambi pia ameandaa mpango wa upimaji ardhi katika kata yake ili kusaidia watu kupata hati miliki za ardhi yao ambapo wananchi 292 wamepimiwa bure ardhi yao na kupewa hati za kimila. Mh. Kunambi alishirikiana na idara ya ardhi kutafuta wafadhili wa kupima mashamba katika kijiji cha Mwarandu. Walifanikiwa kuwapata Haki Ardhi ambalo walifanikisha zoezi hilo. "*Baada ya kugundua kuwa watu walikuwa wanalima mashamba yao bila nyaraka rasmi za umiliki, niliona hii ni kama changamoto kwa sababu kama Serikali ikitaka ardhi katika siku zijazo wao wasingekuwa na la kusema kwa sababu hawana ushahidi wa umiliki. Hilo nililifanyia*

kazi katika vijiji vyote vya kata yangu. Hadi sasa katika kijiji cha Mwalazi mashamba yote/viwanja vyote vimepimwa, na tunangojea hati miliki. Pia tuna wadhamini kutoka Wizara ya Ardhi ambao wametathmini kijiji cha Kibuko na sasa tuko kwenye mpango endelevu wa matumizi ya ardhi".

Changamoto na Mipango ya Baadae

Mh. Mary anasema kuwa mbali na changamoto alizokutana nazo kama alivyoelezea kwenye safari yake, changamoto kubwa aliyokutana nayo ni wananchi kupinga kuanzishwa kwa kata mpya ya Kibuko kwa hofu kuwa watapata tabu ya kujitolea kuchangia ujenzi wa huduma mbalimbali za kijamii katika kata hiyo mpya. *"Nilipambana sana kuhakikisha kata haifutwi. Kwa upande mwingine, itikadi za kisiasa zilinipa changamoto sana. Kati ya vijiji vitatu vya kata yangu, vijiji viwili vilikuwa vinaongozwa na wapinzani. Hivyo, walikuwa hawaungi mkono hoja zangu. Hata hivyo, kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Kibena Kingo na viongozi wa Wilaya niliweza kukabiliana na changamoto hizo."*

Ikiwa atachaguliwa tena kuwa Diwani wa Kata ya Kibuko, Mh. Kunambi atafikiria juu ya kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri lakini tu iwapo Mwenyekiti aliyepo ataamua kutoitetea nafasi yake. "*Nilivutiwa sana na uongozi wa dada Kibena Kingo ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri yetu. Dada Kibena ameonesha ujasiri, ushupavu, na msimamo katika katika nafasi hiyo. Niliweza kufanya kazi kwa karibu sana na dada Kibena nilipokuwa katika kamati ya fedha. Nilijifunza na kuhamasika sana kutokana na uongozi wake."*

Kuwaandaa Viongozi wa Wanawake wa Baadaye

Mh. Kunambi amekuwa akiwatia moyo na hamasa wanawake kugombea katika uchaguzi ingawa mwitikio haujawa mzuri. Anafafanua, "*niliwahaidi wanawake wakijitokeza kuwania nafasi za uongozi nitawanunulia fomu na kuwasaidia kuwanoa ili waweze kubeba ajenda zenye uzito na zinazogusa mahitaji ya wananchi wakati wa kampeni.*" Alifanikiwa kupata wanawake watatu ambao waligombea katika uchaguzi uliopita wa Serikali za mitaa. "*Wengi hawakushinda lakini nina uhakika huu ni mwanzo mzuri, kwa siku zijazo ninatarajia wanawake wengi zaidi kugombea*".

Wito

Mh. Kunambi anawasihi viongozi vijana wa kike kujifunza kuhusu majukumu ya uongozi katika maeneo yao na kujijengea uwezo na ujasiri wa kuongoza wakati wanakua.

Pia, anawaasa wazazi kutotofautisha watoto wa kike na wakiume kwa kuwa wana haki sawa. "*Kama tunavyowafanyia watoto wa kiume/ wanaume, tuwape elimu watoto wa kike/ wanawake na tuwatie moyo pale wanapojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.*"

Mh. Mary amewataka wanasiasa kuungana mkono katika kuleta maendeleo baada ya uchaguzi ili kuharakisha maendeleo katika maeneo yetu badala ya kung'ang'ania itikadi zetu za vyama.

Mwisho, anatoa wito kwa viongozi wa dini kutumia nafasi yao vizuri kubadilisha mitizamo hasi ya jamii juu ya uongozi wa mwanamke. *Anasisitiza,"Maendeleo hayana dini, chama wala itikadi. Ni muhimu kumchagua mgombea kwa kuzingatia uwezo wa kuwaongoza ili kufikia malengo ya maendeleo."*

MH. NDESHUKURWA AKYOO TUNGARAZA

Diwani wa Kata ya Makongo Halmashauri ya Manispaa Kinondoni Mkoa wa Dar es salaam (2015-2020)

"Kuwa katika vyama tofauti vya siasa isiwe sababu yakuwa maadui bali chachu ya kuleta ushindani chanya utakaotuletea maendeleo"

Wasifu

Mh. Ndeshukurwa Akyoo Tungaraza ni Diwani wa kuchaguliwa wa kata ya Makongo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni- mkoa wa Dar es salaam. Alichaguliwa mwaka 2015 na ametumikia nafasi hii mpaka mwaka 2020. Mh. Tungaraza alikuwa ni mmojawapo kati ya Madiwani wanawake watatu wa kuchaguliwa kutoka katika kata 10 za Manispaa hiyo sawa na asilimia 30 ya jumla ya Madiwani wa kuchaguliwa. Halmashauri hiyo ina Madiwani Viti Maalum tano sawa na asilimia 29.4 ya Madiwani wote wa Halmashauri ambao ni 17.

Mh. Tungaraza alizaliwa tarehe 28 Juni 1953 katika kijiji cha Sing'isi, wilaya ya Arumeru mkoani Arusha. Alisoma katika shule ya msingi ya Sing'isi hadi darasa la pili kabla ya kuhamishiwa shule ya msingi Karangai ambapo alimaliza darasa la nne. Alifaulu mitihani yake ya darasa la nne na kuchaguliwa kujiunga na shule ya kati (yaani darasa la tano hadi la saba) katika shule ya Meru Magharibi (kwa sasa inajulikana kama Patandi Chuo cha Elimu maalumu. Wakati alipokuwa darasa la sita aliweza kuongoza kikundi cha shuleni cha maskauti wa kike (Girl Guide) kwenye mazoezi na shughuli nyingine za kiskauti. Baada ya hapo alikwenda kusoma Sayansi kimu kwa miaka miwili huko Kisa Wilaya ya Tukuyu mkoani Mbeya. Katika masomo ya Sayansi kimu, Mh. Tungaraza, alifanya vizuri sana katika masomo yake hasa somo la uuguzi.

Alipata ajira ya moja kwa moja katika hospitali ya Mirembe mkoani Dodoma (1970). Baade 1971 alichaguliwa kujiunga na masomo ya uuguzi katika hospital hiyo hiyo hadi mwaka 1972. Lakini alikatisha masomo kwa sababu mjomba wake aliyekuwa akimgharamia masomo yake aliugua. Wakati akiwa katika hospitali ya Mirembe, alikutana na mwanamke mmoja mgonjwa aliyekuwa anaitwa Elinuru Kaaya aliyeshauri na kumsaidia kuomba nafasi ya ualimu katika Chuo na Ualimu Kabanga- kasulu mkoani Kigoma na kufanikiwa kujiunga na Chuo hicho mwaka 1973 na mwaka 1974 alihamisiwa Mpwapwa Chuo cha Ualimu mkoa wa Dodoma ambapo alihitimu masomo yake mwaka huo huo mwezi Oktoba na kutunukiwa cheti cha ualimu daraja la tatu C. Mnamo mwezi Novemba 1974 Mh. Tungaraza alianza kazi ya kufundisha shule ya msingi Mvumi Makulu iliyopo Dodoma vijijini (kwa sasa inajulikana kama Wilaya ya Chamwino) mkoani Dodoma. Kutokana na elimu yake ya sayansi kimu na ujuzi wa kupika na kushona aliteuliwa kuwa mwalimu kiongozi wa sayansi kimu shuleni pale. Alifundisha katika shule hiyo hadi mwaka 1977 alipoolewa na kuhamia Dar es salaam.

Wakati alipokuwa Chuo cha Ualimu Mpwapwa, alikutana na Felician Tungaraza ambaye alikuwa mfanyakazi wa chuo hicho kama Mkutubi. Felicia Tungazara ambaye kwa sasa anajulikana kama Profesa Tungaraza aliyekuwa mkufunzi kutoka chuo kikuu cha Dar es salaam. Walioana mwaka Septemba 1977 na wamejaliwa kupata watoto wanne ambao ni PHD. Rozalia Tungaraza, Christina Tungaraza, John Tungaraza na Angela Tungaraza.

Mh. Tungaraza alipohamia Dar es salaam kumfuata mume wake aliyekuwa anasoma katika chuo kikuu cha Dar es salaam alipangwa katika Shule ya Msingi Amana wilaya ya Ilala kuanzia 1977 hadi 1979 ambapo alihamishiwa katika shule ya msingi Ilala Kasulu (hadi 1984). Mnamo mwaka 1984 alisafiri kwenda Ujerumani kuungana na mumewe ambaye alikuwa amepata ufadhili wa masomo. Akiwa huko, alisoma cheti cha Lugha ya Kijerumani (1984-1985) huko Boghum na Sayansi kimu (1986-87) huko Augsburg.

Aliporudi kutoka Ujerumani mwezi Octoba mwaka 1988, alihamishiwa kufundisha shule ya msingi Mlimani iliyopo wilaya ya Kinondoni (1988- 1992). Mnamo Mwezi Novemba mwaka 1992 – 1993 ulijiunga na kozi ya kujiongezea ujuzi wa ualimu daraja la 3c kwenda elimu ya sekondari kazini. Mwaka 1997, alijiunga na chuo cha mafunzo ya ualimu daraja la 3A Korogwe hadi 1998 na mwaka 1998/99 alijiunga na Daraja A kwenda diploma. Alipomaliza Diploma aliomba nafasi ya ukaguzi wa shule awali na za msingi tu na kufanikiwa kupata na kupangwa Makao makuu ya elimu Wizara ya elimu na Mafunzo ya Ufundi (1999- 2009). Akiwa katika nafasi ya ukaguzi wa elimu makao makuu aliamua kujiendeleza na masomo ambapo aliomba na kupata nafasi ya kujiunga na

masomo katika chuo kikuu cha Dar es salaam ambapo alisoma shahada ya ualimu elimu ya watu wazima (2001-2005).

Baada ya kuhitimu shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam, aliomba nafasi ya Uafisa Elimu Wilaya katika shule za msingi ambapo alipangiwa kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro mwaka Aprili 2009 - Novemba 2011 alipo hamishiwa katika Halmashauri ya Rombo mkoani Kilimanjaro (2011- Juni 2013). Mnamo tarehe 28 Juni 2013 alistaafu kazi ya kiserikali na ndipo alipoanza kufanya kazi za kisiasa.

Safari ya Uongozi wa Kisiasa

Alipokuwa Dodoma, alijiunga na Umoja wa Vijana wa TANU wilaya ya Dodoma Vijijini (1975-1977). Mwaka 1976, aliteuliwa kuwa Katibu Kata wa UWT katika kata ya Mvumi. Anaeleza, " *Nilikuwa mwalimu kiongozi wa sayansi kimu shuleni, pia nilikuwa Mwalimu wa Mpira wa pete (Netball) shuleni, ikasababisha mimi kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CHANETA (Chama cha Mpira wa Pete Tanzania) Wilaya ya Dodoma vijijini. Tukiwa katika kikao cha kina mama cha wilaya ndipo walipoona uwezo wangu wa kujieleza na kusimama na kujenga hoja mbele ya umati wa watu. Wakaona wanipe cheo ili niweze kusimamia kazi za UWT kata*". Anakumbuka, "*Siku moja wakati nahudhuria mkutano wa UWT kiongozi mwanamke aliniambia wataniteua kuwa kiongozi wa UWT katika ngazi ya kata kwa sababu walipenda jinsi nilivyokuwa nikitoa michango yangu (mawazo) na maoni; Nikakubali*".

Kufanya kazi katika mkoa wa Morogoro kulileta hamasa kwa Mh. Tungaraza katika safari yake ya kisiasa. Anakumbuka aliyoyapitia kule Morogoro na kumfanya atamani kujiunga na siasa. Anasimulia: "*Nilipokuwa kule Morogoro, nilipenda jinsi Madiwani wa upinzani walivyokuwa wakiikosoa na kuishauri Serikali. Nilidhani kwamba naweza pia kufanya hivyo ikiwa nitakuwa kiongozi wa kisiasa siku moja. Hata hivyo, niliamua kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mwaka 2013, hata hivyo niliona nijiiunge na CHADEMA na kuwa nilikuwa mgeni na hivyo isingekuwa rahisi kupata uongozi kupitia CCM wakati upande wa CHADEMA walikuwa na watu wachache na walihitaji viongozi. Nikaona ndio wakati sasa wa kuanza mkakati wangu wa kisiasa.* ".

Mh. Tungaraza alipenda jinsi viongozi wa CHADEMA walivyokuwa wanafanya kazi na kwa kuwaelezea dhamira yake. "*Niliwaambia nataka kujiunga na CHADEMA na kugombea nafasi ya Mwenyekiti katika uchaguzi wa Serikali za mitaa na walifurahi sana.* "

Mh. Tungaraza aligombea katika uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2014 na akashinda nafasi ya Mwenyekiti wa mtaa wa Mbuyuni Kata ya Makongo. Kuboresha upatikanaji wa huduma za maji kwa watu ilikuwa ajenda yake kuu. "*Niliwaahidi watu nitajitahidi kuhakikisha kuwa wanapata maji. Walinipigia kura na nilishinda kwa kishindo. Niliwaambia wanachama wa baraza kwamba tumepewa kazi ya kuhakikisha kuwa maji yanapatikana, lazima tuhakikishe watu wana maji. Tulifanikiwa kukusanya milioni 50 kutoka mradi wa uuzaji wa maji na kuanza kwa kwa kujenga vizimba vya maji kwa wananchi waweze kuchota maji kwa urahisi na ukaribu.Tuliongeza vizimba nane na kufanya kata kuwa na vizimba tisa vya kuchotea maji. Baadaye tukawaunganisha watu mabomba kwa waliohitaji kwa gharama ya Sh. 150, 000 /=*".

Utendaji wa Mh. Tungaraza kama Mwenyekiti wa Mbuyuni uliwashawishi viongozi kutoka mitaa mingine kuona kwamba yeye ndiye chaguo bora kwa nafasi ya udiwani wa kata ya Makongo kwa hivyo walimwendea na kumshauri kugombea nafasi hiyo. Anakumbuka "*Wakati tulipokuwa tukikutana na viongozi wenzangu, waliniambia wanataka mimi niwe Diwani wa Makongo ili niweze kuwasaidia kuleta maji katika kata yote ya Makongo*".

Mh. Tungaraza anapata hamasa kutoka kwa Mh. Halima Mdee (Mbunge wa jimbo la Kawe) na Mh. Esther Bulaya (Mbunge wa jimbo la Bunda). Anasema: "*Halima alikuwa mwanafunzi wangu nilimfundisha Mlimani shule ya msingi. Ninapenda jinsi anavyotoa hoja. Esther Bulaya amekuwa akitumia kila senti yake kuleta maendeleo katika jimbo lake ingawa najua ana upinzani mkali katika jimbo lake kutokana na mfumo dume uliojkita katika jamii, lakini anafanya kazi nzuri*".

Mwaka 2015, Mh. Tungaraza aliomba nafasi ya Diwani kata ya Makongo na aliteuliwa baada ya kupata kura nyingi kutoka kwa wanachama wa chama chake. Alishinda kwa kishindo kura za maoni na kuwashinda wapinzani wake wanaume watatu. Pia, Mh. Tungaraza alishinda kwa kishindo kura za udiwani kata ya makongo ambapo alishinda dhidi ya mpinzani wake kutoka CCM aliyekuwa mwanaume.

Kujenga Ujuzi na Ustadi wa Uongozi

Mh. Tungaraza anaeleza uzoefu wake ulitokana na kuwa Afisa wa elimu huko Morogoro, kupata mafunzo ya TGNP na msingi wa elimu kama mambo muhimu katika mafanikio yake ya uongozi wa kisiasa. Uzoefu wake kama Afisa wa Elimu huko Morogoro ulimfundisha umuhimu wa kutotumia vibaya pesa za umma. Alihoji baadhi ya walimu alipokuwa huko ili kuelewa malalamiko yao na alikuja kujua changamoto zingine ni kwamba walikuwa hawalipwi inavyopaswa wakienda katika likizo, wanaposahihisha mitihani na wanapohudhuria mafunzo. "*Nilikuja kuelewa kuwa suala la pesa ni gumu sana, na lazima uwe mwangalifu nalo*

sana. Nilisema sikuwahi kula pesa za mtu yeyote wakati niko Serikalini kwa hivyo sitakula pesa za mtu yeyote kama kiongozi wa kisiasa. Nilisema ikiwa nitafanikiwa kusimamia pesa za watu vizuri hii itanifanya kuwa kiongozi bora".

Mh. Tungaraza pia amehudhuria mafunzo mbalimbali yaliyoandaliwa na TGNP kwa viongozi wanawake ambayo anasema yamekuwa msaada katika uongozi wake. "*Tulihudhuria mafunzo ya kuandaa wanawake kuwa viongozi. Mafunzo hayo yalikuwa mazuri, ikiwa tungeyapata mapema, tungeweza kuwa bora zaidi. Lakini pia kukaa pamoja na kubadilishana mawazo juu ya kile ambacho wenzako wanafanya ni ni jambo zuri sana. Nakumbuka nimeshiriki katika Vilinge vya Simulizi vinavyoandaliwa na TGNP, ambapo nilipata fursa ya kuwasimulia viongozi wanaochipukia safari yangu ya uongozi kama sehemu ya kushirikishana uzoefu na kuwafunda uongozi vijana wanawake. Kiukweli TGNP ndio shirika pekee ambalo nimeona likiandaa jukwaa kama hili adhimu ambalo linawapa fursa rika mbalimbali kuongea kwa uhuru kama sehemu ya kujifunza, kushirikishana uzoefu na kupanga mikakati ya jinsi ya kujinoa katika nafasi za uongozi*".

Mafanikio ya Utekelezaji wa Ahadi

Ajenda ya 1: Kuboresha Miundombinu ya Barabara

Ahadi muhimu ya Mh. Tungaraza ilikuwa ni "*kufuatilia ukarabati wa barabara ya Makongo na pia barabara za mitaani kama Mlalakuwa, Makongo juu, Mbuyuni na Changanyikeni. Kwa mfano barabara ya kutoka Kijiji cha Yesu (Jesus Village) kwenda Chuo Kikuu ambayo ilikuwa ya msimu na isiyoweza kupitika wakati wa msimu wa mvua*". Anaripoti kuwa barabara ya Makongo haijarekebishwa kwa sababu iko chini ya agizo la wakala wa barabara Tanzania. Barabara za mitaani nyingine zote zinashugulikiwa na chombo kilichoundwa na Serikali kuu ambacho ni TARURA. Barabara kutoka majumba ishirini hadi Mbuyuni kupitia kijiji cha Yesu ilikuwa mbaya sana wakati wa masika lakini kwa juhudi za Mh. Tungaraza na wananchi wa Mbuyuni walijitahidi sana kuikarabati kwa kuchangia na kwa sasa inapitika vizuri muda wote haijalishi ni wakati wa jua au mvua. "*Tulikutana na wanajamii na tukakubaliana kwamba watachangia. Nilipata msaada mkubwa kutoka kwa mume wangu. Alinipa pesa kiasi cha shilingi milioni mbili. Pia nilipata msaada kutoka kwa wananchi mbalimbali wa Mbuyuni. Tulifanikiwa kukusanya jumla ya takribani Shilingi milioni kumi za Kitanzania. Na kwa fedha hizo, tuliweza kukarabati barabara ya kijiji chicho kwa mapande ya lami kwa urefu wa takribani kilomita moja na robo.*

Ajenda ya 2: Kupima na Kuhalalisha Makazi

Mh. Tungaraza aliahidi kufanya juhudi kuhakikisha kwamba viwanja katika kata ya Makongo vinapimwa na kuhalalishwa. Alishauriana na Madiwani wenzake ambao walimwambia ingewezekana kwa sababu shughuli hiyo inafanywa na wataalam waliothibitishwa. Alifanya mikutano na wanajamii katika mitaa husika

kuwaambia juu ya mchakato huo na walikubali kulipia gharama za upimaji wa viwanja vyao. "*Tulianza na mtaa wa Makongo ambapo walipima viwanya vyote na baadhi wameshaanza kupata hati zao za viwanja. Baadaye, tuliendelea na Changanyikeni, Mbuyuni na Mlalakuwa. Na tunaendelea watendaji wa kata na mitaa wanaendelea kuhimiza kwa kasi upatikanaji wa hati za viwanja kwa wananchi wote. Hati zinazotolewa ni hati za kiserikali. Hili ni jambo ambalo ninajivunia kwa sababu halikuwahi kufanyika hapo awali*".

Ajenda ya 3: Kuboresha Usambazaji wa Maji Makongo

Kata nzima ya Makongo sasa inapata maji ya kutosha kutoka DAWASCO, "*Mimi kama Diwani ninawashukuru watendaji wa mitaa na kata kwa sababu walishirikiana bega kwa bega na mimi kuhakikisha tunashirikiana kwa pamoja kupata maji safi katika kata yetu*." Aliendelea na kile alichokuwa akifanya kama Mwenyekiti wa mitaa wa Makongo ili kuhakikisha kuwa watu katika kata wanapata maji safi. *"Tulimuomba Mh. Mbunge atupatie fedha kwa ajili ya kununua pampu ya kupandisha maji Makongo ikanunuliwa. Tulifuatilia Wizara ya Maji, na hadi kufikia mwaka 2017, wizara ikatushauri kuonana na viongozi wa DAWASA kawe na Kimara ambao ndio walisaidia upatikanaji wa maji katika kata yetu. Tulitulikuwa tumeweza kupata maji ya kutosha".*

Ajenda ya 4: VICOBA

Mh. Tungaraza pia ameweza kuanzisha jumla ya VICOBA vinne ambavyo kwa sasa vinafanya kazi katika kata ya Makongo. Vikundi hivyo vina jumla ya wananchama 120, na kwa mwaka kikundi kimoja kina mtaji wa takribani shilingi 84,600,000. Sasa wanawake wanapata huduma za mikopo na kuweka akiba. Anaelezea, "*Niliongea na maafisa kutoka baraza waliokuja kutufundisha, walitupa mafunzo kuhusu mikopo na kuweka akiba pamoja na masanduku ya pesa (vibubu)*". Kupitia vikundi kuna wanawake majenga nyumba, wamenunua bajaji, pikipiki, gari, kufungua biashara mbalimbali kama magenge, mama lishe n.k. kutokana na nidhamu ya pesa wanayojifunza katika kikundi.

Ajenda ya 5: Huduma za Ukusanyaji wa Taka

Mh. Tungaraza anasifika kwa kuanzisha huduma ya ukusanyaji wa taka katika kata ya Makongo, ambayo baadaye baraza la Manispaa iliichukua na kuendelea kuwapatia watu. *"Kabla sijaingia kufanya kazi katika Serikali ya mitaa mtaa wetu ulikuwa mchafu sana. Nakumbuka nilipokuwa Rombo kijijini kulikuwa ni kusafi ajabu. Wanafagia vizuri na kutenga taka ngumu na kavu. Nikashangaa huku mjini tunatupa taka hovyo na hatuoni thamani ya hizo taka. Nikaona sasa tutafute mbinu maeneo yetu yawe masafi na tutafute magari ya kutusaidia kutupa taka. Tulizoa taka na tukafanikiwa. Mwanzoni watu walipokea kwa ugumu sana ikabidi nitoe fedha zangu ili kufanikisha hilo. Baadae, nikaitisha mkutano kupata mrejesho wa kazi ya kuzoa taka na waliona ni jambo jema. Tukawaambia tulitumia fedha zetu. Hivyo, kwa sasa inabidi wananchi nao wachangie zoezi hilo kwa kutoa 3000 kwa mwezi na tukafanikiwa."*

4. Changamoto na Mipango ya Baadaye

Mh. Tungaraza anaitambua barabara ya Makongo ambayo bado haijatengenezwa kama changamoto katika kazi yake ya uongozi wa kisiasa. Anasema: "*Nadhani ujenzi wa barabara hii ni wa kisiasa zaidi kwa sababu fedha zilitengwa tangu mwaka wa 2015. Ukienda TANROAD wanasema pesa za ujenzi ziko, lakini hawana fedha za kulipa watu fidia ambao wataathiriwa na ujenzi.". Changamoto nyingine ni kuitwa wasaliti hasa na vijana ndani ya chama kwa sababu ya kuwa na muingiliano wa kirafiki na wanasiasa na viongozi kutoka vyama vingine vya siasa.* "*Uongozi na kuwa na itikadi tofauti sio uadui au haina maana ya kuwa maadui. Ninajisikia vizuri kukaa na wanachama wa vyama vingine vya siasa kuzungumza, kucheka na kubadilishana mawazo badala ya kujitenga kwa msingi wa kisiasa*".

Mh.Tungaraza hana mpango wa kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sababu ya uamuzi huu ni kile anachokiongelea kama mazingira au urari wa uwanja wa kufanya ya kisiasa hauko sawa kwa makundi mbalimbali katika jamii wakiwemo wanawake na watu wenye ulemavu. "*Kuna uhitaji wa haraka wa kurekebisha uwanja wa siasa ili kutoa fursa sawa kwa watu wote kugombea nafasi mbalimbai za uongozi kama katiba ya Jamhuru ya Muungano wa Tanzania inavyosema, Ibara ya 21 (1) kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria"*

Kuwaandaa Viongozi wa Wanawake wa Baadaye

Mh. Tungaraza amekuwa akifanya michakato ya kuwaandaa viongozi wa siku zijazo. Amewafundisha wagombea wa CHADEMA walioteuliwa kugombea katika uchaguzi wa hivi karibuni wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 kuhusu nini wanaweza kufanya ili kutekeleza na kulinda maslahi ya raia. "*Tulikutana na tukawashauri kwamba wanahitaji kuwa na hoja zenye nguvu, kuweka mbele maslahi ya watu.Tulijaribu kuhamasisha wanawake kugombea na wengi walijitokeza.* "

Wito

Mh. Tungaraza amehimiza kujituma na uwajibikaji wa hali ya juu kwa viongozi, hasa viongozi Wanawake, katika kutimiza ahadi wanazotoa kwa wananchi wao. Pia, Mh. Tungaraza ametoa wito kwa viongozi hasa wanawake kushirikiana katika kutatua changamoto za wanawake na jamii bila kujali itikadi au utofauti wa vyama, '*kuwa katika vyama tofauti isiwe sababu ya kuwa maadui bali chachu ya kuleta ushindani chanya utakaotuletea maendeleo*' anasisitiza Mh. Tungaraza

Vile vile, ametoa wito kwa Serikali na mamlaka husika zinazoshughulikia michakato ya uchaguzi kuboresha uwanja wa ushindani na kuhakikisha makundi yote katika jamii yanapata fursa sawa ya kushiriki katika michakato ya uchaguzi ili kuimarisha demokrasia kwa maendeleo ya taifa letu.

Mh. Tungaraza pia ametoa rai kwa jamii, wadau wa maendeleo na viongozi wanawake katika nafasi mbalimbali kuandaa vilinge vya simulizi ili kutoa fursa kwa rika mbalimbali hususani viongozi wazoefu na viongozi chipukizi, kuongea kwa uhuru kama sehemu ya kujifunza, kushirikishana uzoefu na kupanga mikakati ya jinsi ya kujinoa katika nafasi za uongozi.

MH. ANIPHER KASIMU CHIWILE

Diwani wa kata ya Makuburi Jijini Dar es salaam (2015-2020)

"Jamii inapaswa kutoangalia umri, jinsi au ndoa kama vigezo vya uongozi ila kuangalia uwezo, hekima na busara ili kuweza kupata viongozi mahiri watakaoleta maendeleo".

Wasifu

Mh. Anipher Kasimu Chiwile ni Diwani wa kuchaguliwa wa kata ya Makuburi katika Halmashauri ya Manispaa, Ubungo- jijini Dar es salaam. Alichaguliwa mwaka 2015 na anatumikia nafasi hii mpaka mwaka 2020. Mh. Anifa ni mwanamke pekee kwenye nafasi ya Udiwani wa kuchaguliwa sawa na asilimia 6.3 ya Madiwani wa kuchaguliwa wanawake katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo yenye jumla ya Madiwani wa kuchaguliwa 12. Halmashauri hii ina Viti Maalum vitano sawa na asilimia 31.3. Kwa ujumla Halmashauri ina jumla ya Madiwani 20.

Mh. Anipher alizaliwa katika kijiji cha Kilabu Chini mkoani Kilimanjaro. Alipata elimu yake ya msingi katika shule ya msingi ya Kilabu Chini na ya sekondari katika shule ya sekondari ya Mringa kidato cha kwanza hadi cha nne mkoani Arusha. Baada ya kumaliza elimu ya sekondari alijiunga na chuo cha Teknolojia ya Habari na kozi za Ukatibu Muhtasi/Sekretari. Alihamia Dar es salaam mwaka 1994, ameolewa na Exsaudi Peter Msuya na wamebarikiwa kupata watoto watatu. Familia ya Mh. Anipher inajighughulisha na na biashara ya vifaa vya kielektroniki na vya ushonaji.

Safari ya Uongozi wa kisiasa

Mh. Anipher alipenda siasa tangu utotoni lakini hakushiriki katika kisiasa hadi mwaka 2012. Alivutiwa na mbunge mahiri wa kike Mh. Halima Mdee (Mbunge wa Kawe) na Mh. John Mnyika (Mbunge wa Kibamba) kwa hoja zao makini bungeni. Hivyo, mwaka 2012 alijiunga na siasa na akatafuta uongozi wa kisiasa.

Mh. Anipher alifurahia hoja za kina na zenye ushahidi walizozitoa Mh. Mdee na Mh. Mnyika wakiwasilisha ajenda muhimu wakati wa vikao vya bunge. Anasema kwa mfano Mh. Mnyika alifanikiwa kuchangia na kufanikisha upatikanaji wa maji kati ya mwaka 2010 na 2015 ambapo kwa njia moja au nyingine hoja yake ilichangia katika uboreshaji wa miundo mbinu na upatikanaji wa maji hususani maeneo ya Dar es salaam.

"*Nilijifunza kutoka kwa Mh. Mnyika kwamba ikiwa una ajenda ya kweli, iwasilishe kwa kutoa ushahidi wa kutosha na kutoa mapendekezo, Serikali inasikiliza na inaweza kuchukua hatua. Tangu wakati huo, nilidhamiria kuwa kiongozi wa siasa ambaye anatoa hoja zenye ushahidi kwa sababu nilijua Serikali ingeweza kunisikiliza na kufanyia kazi hoja zangu.* " Anaeleza Mh. Anipher.

Mh. Anipher alijiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mwaka 2012 na kuchaguliwa kuwa Katibu wa tawi kwa mwaka mmoja. Kutokana na utendaji kazi wake, Anipher alipandishwa cheo na kuwa Katibu Kata kwa miaka mitano. Mwaka 2014 wakati akiwa Katibu kata, aligombea nafasi ya uenyekiti wa mtaa lakini hakushinda. Katika uchaguzi alioshindwa ajenda yake ya uchaguzi ilijumuisha maboresho ya barabara, upatikanaji wa maji na miundombinu ya afya.

"*Watu walizipenda ajenda zangu na kuziona ni za muhimu. Hata hivyo, walikuwa na mashaka kuhusu umri wangu.Walidai nilikuwa mdogo sana kuweza kusikiliza na kutatua matatizo yao ya ndoa. Ilionekana kwamba kuelewa na kutatua matatizo ya ndoa lilikuwa ni jukumu la muhimu la Mwenyekiti wa mtaa, hivyo walitaka lifanywe na mtu mzima. Hivyo, walimchagua mgombea mtu mzima wa kiume na mwenye uzoefu*". Anasema Anipher na kuongezea, "*…kwangu mimi haikuwa hasara kabisa. Ilikuwa kama ushindi kwa sababu kampeni ya uchaguzi ilinipa fursa ya kujulikana na kujitathmini. Watu walinijua na baadhi waliamini nilikuwa naweza na waliniahidi kuniunga mkono katika siku zijazo".*

Kutokushinda katika uchaguzi hakukumzuia Anipher kukitumikia chama chake na watu. Aliendelea kutumikia watu kama kiongozi wa chama. Wajumbe wa chama chake cha siasa waliridhika na utendaji wake. Wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, watu hao hao walimshawishi agombee nafasi ya udiwani wa kata ya Makuburi. Walitaja kazi nzuri ambazo alikuwa akifanya kama kiongozi wa chama na walidhani anaweza kufanya vizuri zaidi katika nafasi hiyo. Alisita kwa sababu alifikiria kwamba nafasi hiyo ilikuwa ya juu sana na yenye majukumu mengi na mazito. Anakumbuka jinsi mwanamke mmoja na kiongozi wa chama chake cha siasa alivyomfuata na kumwambia, "*Mwanangu hakuna nafasi kubwa au ndogo. Uwezo na kujitolea kuwatumikia watu ndio jambo la muhimu zaidi. Nakuona una vigezo muhimu na tayari umeonesha upendo wako na utayari kuwatumikia watu wa Makuburi. Jiamini katika uwezo wako na uchukue nafasi, tutakusaidia*".

Maneno hayo yalimtia sana moyo Mh. Anipher na alikubali kugombea nafasi ya udiwani. Aligombea pamoja na wagombea wengine tisa katika uchaguzi wa awali wa chama na akashinda. Aliteuliwa rasmi kuwa mgombea wa CHADEMA kushindana dhidi ya wagombea wanane kutoka vyama vingine vya siasa. Alipanga mkakati bora wa kampeni, alifanya kampeni kwa ustadi, na mwishowe akaibuka mshindi na kutangazwa kuwa Diwani wa Kata ya Makuburi.

Ajenda za Uchaguzi na Mikakati ya Kampeni

Ajenda ya uchaguzi na mkakati madhubuti wa kampeni ni funguo za kushinda uchaguzi. Anipher alilazimika kutambua na kuwasilisha vizuri mambo ambayo angefanya na kurekebisha endapo atachaguliwa. Anasema kwamba kutambua ajenda sahihi za uchaguzi kunahitaji utafiti na mashauriano mengi. *"Ilinibidi niende kuzunguka mitaa yote ya kata ya Makuburi kuwauliza watu changamoto zao kuu ni nini na walitaka nifanye nini. Masuala yaliyoangaziwa zaidi yalikuwa ni kujenga ofisi ya kata, kuboresha barabara za mitaa, kusambaza maji ya bomba, kuboresha huduma bora za afya na ukarabati wa shule. Katika masuala haya yaliyopewa kipaumbele niliongeza michezo kwa vijana*", anaelezea.

Mh. Anipher alilazimika kupanga mikakati ya kushughulikia mambo yaliyopewa kipaumbele hapo juu na kuyawasilisha vizuri wakati wa mkutano wa kampeni. Anakumbuka, "*Niliona mikutano ya kampeni kama fursa kwangu kuelezea wazi ajenda zangu na kuonesha njia za kuzifanyia kazi.*

Kwa hivyo, niliwaambia wasikilizaji kuwa nitashirikisha kila mkazi, Afisa wa Serikali, kiongozi wa Halmashauri na wataalam katika kutafuta suluhisho la kila changamoto katika Kata. Nilisisitiza kwamba niko kuwahudumia na kwa hivyo nimeazimia kufanya kila kitakachowezekana ili kuwezesha idara za Halmashauri ya Manispaa kutimiza majukumu yao na kutoa huduma bora kwa wakazi wangu. Niliongeza kwamba nitaangalia kila fursa na kubisha kila mlango kutafuta msaada ili kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi ya wakazi wa Makuburi. Nilihisi kwa hakika kuwa taratibu wapiga kura walianza kupata ujumbe wangu na kila siku idadi ya watu waliohudhuria mikutano yangu ya kampeni ilikuwa ikiongezeka".

Mh. Anipher alikuwa na hamu ya kujenga mkakati madhubuti wa kampeni. "*Nilijua haitoshi kuwa na ajenda ya uchaguzi inayofaa. Mbinu ya kampeni yenye nguvu na madhubuti inahitajika kuondokana na uwezekano wa vizuizi vyovyote vile. Kama mgombea wa kike, nilijua nina vizuizi zaidi vya kuvishinda katika safari yangu. Kwa hivyo, tuliamua kuunda timu bora ya kufanya kampeni na kuipangia majukumu ya kuchambua masuala yaliyowasilishwa na wagombea wenzangu na kupanga mkakati juu ya majibu madhubuti ya masuala kama hayo. Tulikubaliana pia na mume wangu aandamane nami kwenye mikutano ya kampeni ili kupinga uvumi kwamba mimi ni mwanamke ambaye sijaolewa na asiye na maadili au kwamba sina*

msaada kutoka kwa familia yangu. Kwa kuongezea, tulikuwa na kamati ya hiari ya wazee wenye kuheshimiwa ili kuniunga mkono na kuonesha kuniamini hasa wakati ugombea wangu ulipohojiwa kwa misingi ya jinsi na umri". Anafafanua.

Mkakati wa kampeni wa Anipher ulizaa matunda kama jinsi anavyosema, "*wajumbe wa timu yangu ya kampeni walitembelea mikutano ya kampeni ya wagombea wengine, walikusanya taarifa nyingi, wakachambua na kupendekeza majibu sahihi kwa propaganda. Kwa mfano, kupingana na propaganda kwamba nilikuwa msichana mchanga na asiye na adabu na sikuwa na msaada wowote kutoka kwa familia yangu, timu ilipendekeza kwamba mume wangu na wazee wengine wenye kuheshimiwa waandamane nami kwenye mikutano na wapewe nafasi ya kuongea kuonesha kuniunga mkonona kuniamini. Wapiga kura wengi walifurahia sana kumuona mume wangu na kujua kuwa ananiunga mkono na pia waliona jinsi wazee wanavyounga mkono ugombea wangu kwa msingi wa uwezo wangu wa kutimiza ahadi*".

"*Mbali na hilo, wataalamu wa kampeni za kisiasa na mawasiliano katika timu yangu walitathmini hotuba zangu za kampeni mara kwa mara na kunielekeza kuzingatia kuelezea ajenda yangu na mikakati ya utekelezaji badala ya kufanya propaganda na siasa rahisi za kushambulia na kuchafua wagombea wenzangu. Nilifuata ushauri wao wa kitaalam na wakati wote wa kampeni, nilipokelewa vyema na wapiga kura wengi waliodai kutaka kujua sera na mikakati ya wagombea kwa ajili ya kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi katika eneo na sio masuala yasiyo na msingi yanayohusisha masuala ya kibinafsi* ", anaongezea.

Anipher anatambua msaada mkubwa ambao aliupata kutoka kwa watu binafsi, vikundi vya kijamii na taasisi wakati wa kampeni zake. "*Nimejenga uhusiano mzuri sana na viongozi wangu wa chama, wafanyabiashara na vikundi vya wanawake. Wakati wa kampeni, wote hawa waliamini kwamba nina uwezo wa kuwa mwakilishi mzuri wa watu hivyo wakanipa misaada ya aina mbalimbali. Walinipa usafiri, na msaada wa hali na mali*".

Kujenga Ujuzi na Ustadi wa Uongozi

Mh. Anipher anafahamu kwamba ili kutekeleza ahadi za uchaguzi inabidi mtu awe na uwezo sahihi na ufahamu wa uongozi bora. "*Kama kiongozi mwenye umri mdogo katika siasa, nilijua sikuwa na ufahamu na ujuzi wote wa kujihusisha na viongozi wa Serikali na kushiriki kikamilifu katika vikao na shughuli za baraza. Nilikuwa na bahati kushiriki warsha na mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa ya Hombolo wakishirikiana na TGNP. Kutoka kwenye mafunzo, nilijifunza jinsi ya kuuliza maswali ya muhimu, kutoa hoja zangu zenye ushahidi na kufuatilia ahadi za misaada zilizotolewa na makubaliano kuhusiana na mambo yaliyojadiliwa katika Kata. Pia nilijifunza kuhusu kutengeneza mipango na bajeti. Hayo yalinijengea kujiamini na ujasiri*".

Anipher anashukuru kwa fursa zote alizopata ili kufungua na kuimaisha uwezo wake wa uongozi. Sasa anajiamini na anaweza kuwasiliana na mtu yeyote katika kutekeleza ahadi zake. Anaelezea jinsi anavyowasiliana na watu wa kawaida, wataalamu, idara za Serikali na sekta binafsi katika kutekeleza mipango yake kama inavyoelezewa hapo chini katika kufanikisha kutatua baadhi ya changamoto katika Kata.

Mafanikio ya Utekelezaji Ahadi za Uchaguzi

Ajenda ya 1: Ugavi wa Maji Safi

Anipher aliwaza kuhusu upungufu wa maji ya bomba kwenye kata yake. Wakazi wengi walikuwa wanapata maji yasiyo salama kutoka katika visima vilivyochimbwa kwa mkono. Akaamua kufuatilia katika shirika la maji ambalo hutoa huduma ya maji katika mikoa ya Dar es salaam na Pwani (DAWASCO) ili kuulizia uwezekano wa kupata maji ya bomba katika kata ya Makuburi. Baada ya siku kadhaa, Meneja wa DAWASCO alitembelea eneo lake ili kutathmini hali halisi; wakaamua kutengeneza bomba jipya. Nyumba zote zilifanikiwa kupata maji ya bomba na wenyeji wakawa wanapata maji safi na salama.

Ajenda ya 2: Ujenzi wa Ofisi wa Kata

Kwa muda mrefu, kata ya Makuburi imekuwa haina ofisi za kudumu kwa ajili ya wafanyakazi wake na viongozi. Mh. Anipher aliwaahidi wakazi kuwa atahakikisha kwamba ofisi ya kata inajengwa kwa wakati muafaka. "*Katika mkutano wangu wa kwanza na wajumbe wa baraza la kata, nilieleza nia yangu ya kuiomba Serikali iniunge mkono katika ujezi wa ofisi ya Kata. Wajumbe wa kata waliniunga mkono. Tukaweka katika mipango ya maendeleo. Wakati huo huo, nikamtafuta msanifu wa majengo na mkazi wa Makuburi na kumuomba atusaidie kutengeneza muundo wa ofisi. Akatengeneza muundo mzuri bila malipo. Nikauwasilisha kwa wahandisi wa baraza la Halmashauri ambao waliupenda na baadae ulipata kibali cha baraza hilo. Tulipata kiasi cha shilingi milioni tisini na sita za kitanzania kwa ajili ya ujenzi wa ofisi. Ujenzi huo ulikamilika na nina furaha kwamba wafanyakazi wa kata na wakazi wanatoa na kupata huduma ipasavyo kupitia ofisi hiyo*".

Ajenda ya 3: Ujenzi na Ukarabati wa Madarasa na Vyoo

Wakati wa kampeni, Mh. Anipher aliahidi kuboresha hali ya madarasa na vyoo katika umma za shule za msingi na sekondari katika kata ya Makuburi. Hapakuwa na madarasa ya kutosha na vyoo katika shule nyingi za umma zilizopo katika kata hiyo. Baadhi ya madarasa na vyoo vilihitaji matengenezo kwa sababu vilikuwa katika hali mbaya.

"*Baada ya uchaguzi, nilitembelea shule zote katika kata yangu na niliona mapungufu katika madarasa na vyoo. Nilipeleka taarifa hizi kwa kamati ya maendeleo ya Kata ambapo niliwaomba wajumbe waipe taarifa hii kipaumbele. Wajumbe walikubali. Tuliiandika taarifa hiyo inayoonesha idadi ya madarasa na vyoo vilivyohitajika na vile vilivyohitaji ukarabati. Tuliipeleka taarifa hiyo na kuomba fedha toka kwa baraza la Manispaa. Tulipewa shilingi milioni thelathini na mbili kwa ajili ya kukarabati vyoo katika kila shule ya msingi ya Serikali. Tumeweza kukarabati madarasa manne ya shule ya msingi Makuburi, madarasa sita ya shule ya msingi Mabibo, na madarasa mawili ya shule ya sekondari Makamba. Pia tumeweza kujenga madarasa manne ya shule ya msingi Makoka na madarasa manne katika shule ya sekondari Makamba. Kuongezea, tumepata ufadhili wa shilingi milioni arobaini na saba kutoka Songas na zimetumika kujenga madarasa mawili katika shule ya msingi Kisiwani*".

Ajenda ya 4: Utoaji wa Madawati na Vifaa vya Maabara katika Shule

Suala lingine ambalo Mh. Anipher alipaswa kulishughulikia kila mwaka ni upungufu wa madawati na vifaa vya maabara vya kutosha katika shule za umma. Kufuatia utekelezaji wa ajenda ya elimu bure, kila mwaka katika shule mbili za sekondari na sita za msingi katika kata yake ziliandikishwa wanafunzi wengi ambayo ililazimu kuhakikisha kama uwepo wa madawati na vifaa vya maabara ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi waliongezeka. "*Ninajua Halmashauri ya Manispaa inatoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara; kazi yangu ilikuwa ni kufuatilia. Nilitembelea shule mbalimbali na kuangalia vifaa vya maabara vinavyohitajika na kuripoti kwa mamlaka za Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji. Halafu niliendelea kufuatilia mpaka fedha zilipotolewa na vifaa kununuliwa. Kuhusu madawati, kila mwaka niliomba msaada kutoka kwa wakazi na mashirika binafsi kwa ajili ya kutoa madawati. Kwa miaka mitatu, tumekuwa tunapata michango ya kifedha kutoka kwa wasamaria wema na makampuni na kuzitumia kutengeneza madawati mapya*".

Ajenda ya 5: Upanuzi wa Vituo vya Afya

Kuboresha vituo vya afya na utoaji wa huduma bora za kiafya zilikuwa ni ajenda muhimu za Mh. Anipher. Kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali katika kata yake, Mh. Anipher aliwasiliana na mamlaka ya Serikali inayosimamia na kutekeleza sera ya Serikali kuhusu kukuza kanda maalum ya uchumi (Export Processing Zones Authority-EPZA). Mamlaka hii ipo katika kata yake. *"Tuliandika barua EPZA na kupata majibu mazuri. EPZA waliainisha kwamba wangeweza kutusaidia*

kama sehemu yao ya uwajibikaji kwa jamii inayowazunguka. Waligharamia ujenzi wa jengo la kliniki ya uangalizi na matibabu; na ukuta wa uzio wa kuzunguka kituo cha afya kwa ajili ya ulinzi. Eneo letu la nje kwa ajili ya kituo cha afya lilikuwa dogo kuweza kufanyiwa upanuzi zaidi. Hivyo tuliwafuata kikosi cha Polisi Tanzania na kuwaomba ekari kumi za eneo lao ili tuweze kujenga kituo kipya cha afya. Kikosi kilikubali na kutupa ekari tano za ardhi eneo la Makoka, mipango inaendelea kuhamasisha kutafuta rasilimali kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha afya".

Changamoto na Matarajio ya Baadae

Mh. Anipher anaridhishwa na yale ambayo amefanya na kufanikisha mpaka sasa. Anaamini wakazi wengi wa Makuburi wanaridhishwa pia. "*Watu wengi wanafurahi na kupendezwa na mambo ambayo nimeweza kuyafanya. Huwa wananipigia kunipa pongezi kwa ajili ya mafanikio maalum na kuahidi kuendelea kuniunga mkono. Hilo linanipa nguvu ya kuendelea kuwatumikia*".

Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Mh. Anipher pia anapitia changamoto. "*Changamoto kubwa zinahusiana na mitazamo na uelewa finyu wa masuala ya kijinsia. Bado baadhi ya watu hawaamini katika uwezo wa viongozi wanawake na wanaendelea kusita kuunga mkono ajenda yangu ya maendeleo. Changamoto nyingine ni matarajio ya yasiyotekelezeka ambayo watu wanayo kwa viongozi wao. Baadhi ya watu wanategemea viongozi wao wawape fedha ili kutatua matatizo yao au kuwatembelea mara kwa mara majumbani kwao. Ukweli ni kwamba fedha ni changamoto, ni vigumu kupata hela za kuwapa watu. Vile vile, sio rahisi kupata muda wa kuwatembelea watu mara kwa mara majumbani mwao. Ninaelewa hizi changamoto na nisingependa kuahidi kitu ambacho sina uwezo nacho na sitaweza kutekeleza'*.

Mh. Anipher tayari ana ndoto kubwa. Anatamani nafasi ya juu ya kuhudumia jamii kuliko ile ya Udiwani. "*Nina ndoto ya kuwa mbunge ili niweze kusaidia jimbo kama ninavyosaidia kata yangu sasa. Inaweza isitokee hivi karibuni lakini, Mungu akipenda, itatokea katika siku zijazo*".

Wito

Mh. Anipher anatoa wito kwa vijana hususani Wanawake kutokukubali kukatishwa tamaa, kujitokeza kwa wingi katika nafasi za uongozi na kuwa pindi wanapopata nafasi hizo wazitumie vizuri kwa kufanya kazi kwa bidii kuithibitishia jamii kuwa vijana, wanawake wanauwezo mkubwa wa kuongoza hivyo wapewe nafasi. Kwa upande mwingine, Mh. Anipher ametoa wito kwa jamii kutoangalia umri, jinsi au hali ya ndoa kama vigezo vya uongozi, ila kuangalia uwezo, hekima na busara.

MH. HELGATIEL MCHOMVU

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai na Diwani wa Kata ya Muungano Mkoani Kilimanjaro (2015-2020)

"Wanawake jitokezeni kugombea msisubiri nafasi za Viti Maalum. Najua na ninaamini mna uwezo mkubwa wa kuongoza kwa sababu mmethitisha kuwa viongozi mahiri kuanzia ngazi ya familia".

Wasifu

Mh. Helgatiel Mchomvu ni mojawapo wanawake wenyeviti watano tu wa Halmashauri 185 zilizopo Tanzania bara anayeongoza Halmashauri ya Hai. Pia, Mh. Mchomvu ni diwani wa kata ya Muungano ndiye Diwani mwanamke wa kuchaguliwa katika Halmashauri ya Hai yenye jumla ya Madiwani wa kuchaguliwa 17. Halmashauri hiyo ina Madiwani Viti Maalum sita sawa na asilimia 26 ya Madiwani wote wa Halmashauri (23).

Mh. Helgatiel Mchomvu alizaliwa katika kijiji Olmolock katika wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro. Alipata elimu yake ya msingi Sanya Juu shule ya msingi mwaka 1970 -1976 na sekondari ya wasichana Masama kuanzia kidato cha kwanza hadi cha pili (1977-1978 mkoani Kilimanjaro. Mh. Helgatiel anakumbuka jinsi alivyoweza kuwapanga wanafunzi wenzake kudai chakula bora alipokuwa mwanafunzi wa kidato cha pili mwaka 1978. Alihamia shule ya Sekondari Arusha Meru na kumalizia masomo yake ya sekondari. Mh Helgatiel alishika uongozi wa wanafunzi yaani kiranja akiwa shule ya msingi na sekondari pia.

Baada ya kumaliza masomo yake ya sekondari mwka 1983 aliajiriwa na uwanja wa ndege wa Kilimanjaro katika idara ya usalama kama mlinzi wa kawaida. Alijiendeleza na mafunzo ya ulinzi na kupata cheti za ulinzi ngazi ya 3. Alifanya kazi huko kwa miaka kumi na moja (11) hadi mwaka 1994 alipostaafu kwa hiari na kuanza biashara yake.

Safari ya Uongozi wa Kisiasa

Mh. Helgatiel alijiunga na CHADEMA mnamo mwaka 1992 kama mwanachama wa kawaida. Mara baada ya kustaafu kwake mwaka 1994, aliombwa na rafiki yake kuwa kiongozi wa CHADEMA katika nafasi ya Mwenyekiti wa wanawake (Wilaya ya Hai). Anakumbuka "*Nilisita kwa sababu sikuwahi kuwa kiongozi na sikupendelea sana kuzungumza kwenye umati hususani masuala ya kisiasa. Baadaye nilikubali ombi lake baada ya vitendo vingi vya ushawishi. Nilitambulishwa kwa watu wawili (marehemu Kabigi na Nkomola) ambao walinitia moyo na kunifundisha jinsi ya kuongea katika mkusanyiko wa watu mpaka nikapata uzoefu*".

Baada ya kupata uzoefu, Mh. Helgatiel aligombea na akashinda nafasi ya Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya (Wilaya ya Hai) mnamo mwaka 2000 ambapo alishinda dhidi ya wanaume wawili.

"*Nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Madiwani Tanzania mwaka 2005-2010 ambapo nilishinda dhidi ya wagombea wawili, mmoja wa kiume na mwingine wa kike. Pia, kwenye chama niligombea nafasi ya ukatibu mwenezi wa chama ambapo nilishinda dhidi ya mwanaume mmoja nikawa Katibu Mwenezi wa mkoa (2005-2010) na wakati huo huo niligombea nafasi ya ukatibu mwenezi wa baraza la wanawake la taifa nikashinda dhidi ya wanawake wanne*".

Mnamo mwaka 2010, aligombea bila mafanikio ya nafasi ya ubunge wa jimbo la Same mkoani Kilimanjaro. Kama Katibu wa chama wa mkoa, Mh. Helgatiel alikuwa ameamua kusimama katika jimbo hilo licha ya kwamba hakuwa na mizizi kwa sababu chama hicho hakikuwa na mgombea katika jimbo hilo. Katika uchaguzi huo kulikuwa na wagombea saba (7) kutoka vyama saba vya siasa, CCM ilishinda na CHADEMA ikawa ya tatu.

"Ingawa watu wengi walinitaka nigombee Udiwani wa Kata nilikataa kwa sababu sikuwa nimejiandaa badala yake nilipata mtu mwingine ambaye aligombea nafasi hiyo na akashinda. Niliteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum kwa mara ya tatu. Kuanzia wakati huo, nilianza kujiandaa kwa kugombea katika uchaguzi ujao kama Diwani wa Kata. Itakumbukwa kuwa kwa wakati huo nilikuwa nimegombea ubunge wa Viti Maalum katika chama; ingawa nilishinda kwa kura nyingi kuliko wanawake wengine (kwa mihula mitatu mfululizo) sikuwahi kuteuliwa kutokana na maamuzi ya viongozi".

Mnamo mwaka 2015, Mh. Helgatiel aligombea na kushinda nafasi ya Diwani wa Kata ya Muungano, akiwashinda wagombea wengine watatu (wote wanaume) kutoka vyama vingine vya siasa. Hata hivyo, ilibidi kwanza kuushinda upinzani mkali kutoka ndani ya chama ili kushinda kura za uteuzi wa chama. *"Mchakato ulianza na kura za uteuzi katika chama ambapo tulikuwa wagombea watatu; wanaume wawili na mimi. Kama kawaida wanawake tunakutana na vikwazo vingi*

katika kugombea nafasi za uongozi kwa viongozi hususan wanaume. Kulikuwa na dalili zote za viongozi wangu kuunga mkono wagombea wenzangu wale wanaume. Katika kura za uteuzi, nilishinda asilimia 80 ya kura na wagombea wengine walishiriki asilimia iliyobaki".

Licha ya upinzani na changamoto alizokutana nazo kutoka katika chama chake mwenyewe, aliweza kuwasilisha fomu za uteuzi za Tume ya Uchaguzi (NEC) na mwishowe akaendelea na kampeni za uchaguzi mkuu. "*Wakati wa kampeni, nilifanya kampeni ya mtaa kwa mtaa, mtu baada ya mtu na nyumba kwa nyumba na timu yangu ya watu watano. Mwishowe, niliwashinda washindani wangu, wanaume wawili, kwa kishindo cha kura 2830.*"

Mwaka 2015, Mh. Helgatiel aligombea na kushinda nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kati ya mgombea mmoja wa kiume. Hata hivyo, kama katika chaguzi zilizopita, anaelezea kwamba kushinda nafasi hio haikuwa kazi rahisi pia. "*Ilikuwa ngumu sana huko. Kijana mdogo ambaye aligombea alikuwa na pesa nyingi na alikuwa mpya katika chama hivyo alitumia pesa nyingi kuwapa rushwa Madiwani. Wakati sisi Madiwani tulipopiga kura alishinda kwa kura tatu au nne lakini nilimshinda katika kura za kamati ya chama ya wilaya. Baada ya hapo, Kamati ya Kitaifa iliniteua kuwa mgombea wake kugombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri*".

Kujenga Ujuzi na Ustadi wa Uongozi

Mh. Helgatiel anasisitiza kwamba uongozi bora unahitaji kuwa na ujuzi muhimu. Anafikiria kuwa uwezo wake wa uongozi ni wa kuzaliwa na umejengwa zaidi kutokana na mafunzo kutoka TGNP na ICLD. '*Kupitia TGNP niliweza kushiriki mafunzo ya uongozi pamoja na bajeti yenye mrengo wa kijinsia yaliyonisaidia katika kampeni na michakato mbalimbali ya uchaguzi pamoja na katika kutekeleza mipango yangu ya kuwatumikia wananchi. Katika nafasi yangu kama Mwenyekiti wa Halmashauri niliweza wafundisha Madiwani wenzangu juu ya umuhimu wa kutenga bajeti zenye mrengo wa kijinsia*'.

Mafunzo na uchapakazi wa Mh. Helgatiel ulizidi kumpa ujasiri wa kuendelea kugombea nafasi mbalimbali na wakati huo huo kuweza kushinda nafasi mbalimbali, kulizidi kumpa hamasa ya kuendelea kugombea nafasi mbalimbali kama alivyoelezea hapo juu kwenye safari yake ya uongozi. *"Ushindi wangu wa mara kwa mara ni ushahidi kuwa jamii inafurahia uongozi wangu. Najivunia sana kushiriki katika kujenga chama ikiwemo kuwavuna wanachama wengi kujiunga na chama chetu".*

Mafanikio ya Utekelezaji Ahadi za Uchaguzi

Ajenda muhimu ya uchaguzi ya Mh. Helgatiel ilijumuisha ujenzi wa mtandao wa barabara kwa sababu Muungano ilikuwa kata mpya, kujenga shule, na kusambaza maji haswa kwa ajili ya shule katika maeneo ya jamii ya Wamasai.

Ajenda ya 1: Ujenzi wa Barabara

Mh. Helgatiel pamoja na viongozi wengine wa Serikali waliweza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu mpya katika kata ambayo imeongeza thamani ya ardhi na bei ya viwanja katika eneo hilo. Barabara ilijengwa kupitia fedha kutoka katika bajeti ya kawaida ya baraza kama anavyofafanua "*Niliwasilisha wazo kwa baraza, nikaongea na kumshawishi Mhandisi wa Wilaya na kisha fedha zikatengwa kwa ajili ya ujenzi. Ujenzi wa barabara zingine unaendelea*".

Ajenda ya 2: Ujenzi wa Shule Mpya

Kupitia uongozi wa Mh. Helgatiel, shule mpya ya msingi katika kata ilijengwa na kukamilika, shule hiyo inajulikana kama shule ya msingi Kambi ya Raha. Madarasa mengine matatu zaidi yamejengwa katika shule hiyo. Hata hivyo, ahadi yake ya kujenga shule nyingine katika eneo la jumuiya ya wamasai bado haijatimia. "*Kulikuwa na eneo huko Maasailand ambapo tulipanga kujenga shule mpya, lakini hatujafanikiwa kwa sababu ya kutoelewana na viongozi wengine wa kisiasa na Serikali. Hata hivyo, bado ninaendelea na mpango huo*". Chini ya uongozi wake, Baraza limeweza kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kuwasaidia watu wenye ulemavu, vijana na wanawake kupitia mikopo, akitolea mfano mwaka 2018 ambapo shilingi milioni 30 zilitolewa na kunufaisha vikundi vya ufugaji, kilimo cha mboga mboga na upandaji miti.

Changamoto na Mipango ya Baadae

Mh. Helgatiel anaripoti changamoto nyingi ambazo anakabiliana nazo katika majukumu yake ya sasa ya uongozi ambayo yanaathiri vibaya utekelezaji wa ahadi zake za uchaguzi. Kulingana na Mh. Helgatiel kuna mipango kadhaa ambayo imeshindikana kutokana na utofauti wa itikadi za kisiasa

Katika mipango yake ya baadae, Mh. Helgatiel anatarajia kujikita kwenye jimbo kupitia ubunge wa Viti Maalum ili kuandaa njia kwa ajili ya kugombea ubunge wa kuchaguliwa. Lengo lake kuwa la kutaka kushika nafasi hiyo, Mh. Helgatiel anasema ni kupata fursa ya kuendelea kuhamasisha kina mama kwenye biashara na mitaji ili kujikwamua kiuchumi na kuweza kuingia pia katika siasa.

Wito

Mh. Helgatiel anaamini kuwa wanawake wanaotamani kuwa viongozi wanapaswa kuangalia hadithi za kisiasa na za uongozi za viongozi waliofaulu ili kujifunza na kutiwa moyo. "*Kabla ya kuwa kiongozi, sikujua hata kidogo juu ya siasa na nilikuwa nasita kuchukua fursa za uongozi Nilikuwa na hofu mwanzoni lakini sasa nimejifunza kuwa jasiri kwa kile ninachofanya*". Pia anasisitiza kuwa maendeleo hayana chama. Baada ya uchaguzi ni muhimu kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali katika kutekeleza mipango ya maendeleo bila kujali itikadi za vyama. "*Wanawake wajitokeze kugombea wasisubiri Viti Maalum, nina amina wana uewezo mkubwa kuongoza kwa sababu tangu chimbuko ni viongozi kuanzia ngazi ya familia", anahitimisha.*

Kwa Taarifa Zaidi

Mtandao wa Jinsia Tanzania
Mabibo Dar es saalam
S.L.P 8921
Simu: +255 754 784 050
Barua Pepe: info@tgnp.or.tz
Tovuti: www.tgnp.or.tz

@tgnptz1 @tgnptz